


**SIMBA SC, YANGA SASA NI SHUSHA NISHUSHE**
UKURASA 24

**TRA** yaandika rekodi nyingine ya makusanyo
UKURASA 3

**MJAMZITO** afariki dunia akidaiwa kunyimwa huduma hospitalini
UKURASA 5



**RAIS** Dk. Mwinyi kurejesha usafiri wa treni Zanzibar
UKURASA 17


# Nipashe

Jumanne Januari 2, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581543

www.ippmedia.com

LIKE & FOLLOW US
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper


## HOFU YA VIRUSI

# Malori 24 yenye soya yazuiwa kuingia nchini

**WIKI** mbili yako mpakani yakitokea Malawi...*Endelea ukurasa 16*



Watoto wakiogelea katika bwawa la maji katika kusherehekea Sikukuu ya Mwaka mpya mjini Muheza mkoani Tanga jana.
**PICHA: STEVEN WILLIAM**

UKURASA WA 24

## KOCHA STARS ATEMA CHECHE, AKIANIKA MAJEMBE YA AFCON



KOCHA Mkuu wa Taifa Stars, Adel Amrouche, amefunguka juu ya kuwaita wachezaji ambao hawapati nafasi katika timu zao akiamini wanauwezo wa kuonyesha maajabu...

## Mvua kubwa kushuka mikoa mitano kesho

UKURASA 5

# Maaskofu: Njia ni hii 2024

UKURASA 2

**MICHEZO** **OKRAH KUANZA YANGA NA WASUDAN MAPINDUZI LEO** UK. 23

**KATUNI** UK. 6

# Maaskofu: Njia ni hii mwaka 2024



Makamu wa Rais, Dk Philip Mpango akishiriki katika ibada ya Mwaka Mpya na waumini wengine katika Kanisa Katoliki Parokia ya Mwenyeheri Maria Theresa Ledochowska Kiwanja cha Ndege Dodoma jana. **PICHA: OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

**Na Waandishi Wetu**

WAKATI watanzania wakisherehekea Sikukuu ya Mwaka Mpya, viongozi wa dini wamewataka wazazi na walezi kuwalea watoto katika maadili na kuwalinda dhidi ya mitandao ya kijamii.

Pia wamewataka watanzania kuepuka mikopo yenye masharti magumu, maarufu kausha damu pamoja na kuepuka fitina, majungu na chuki, badala yake waishi kwa upendo na amani.

**FITINA, CHUKI**

Askofu wa Kanisa Katoliki Jimbo la Shinyanga, Mhashamu Liberatus Sangu, ndiye aliwataka watanzania kumtanguliza Mungu kwa kila jambo katika Mwaka Mpya wa 2024, kuacha fitina, majungu, chuki na kuishi kwa upendo na amani.

Akitoa neno wakati wa misa ya mkesha wa Mwaka Mpya iliyofanyika katika Kanisa Katoliki Parokia ya Ngokolo ya Mama Mwenye Huruma mjini hapa, Askofu Sangu alisema watanzania wanapaswa kuishi kwa amani na upendo.

Alisema mwaka huu uwe wa amani, watu waishi kwa upendo na kuacha kufanyiana fitina, majungu na chuki na kwamba vyote hivyo vinawezekana ikiwa watamtanguliza Mungu kwa kila jambo.

Kiongozi huyo wa kiroho alitoa wito kwa watanzania kuishi kwa kumshukuru Mungu na kuwa na moyo wa shukrani ili wapate neema kwa kuwa kuumaliza mwaka si jambo la mchezo.

"Wengi wametangulia mbele za haki na si kwamba sisi tuliobaki ni wakamilifu, la hasha! Hivyo ni vyema kuishi kwa kumshukuru Mungu kwa kila jambo kwani kila linalotokea ni mipango ya Mungu," alisema Askofu Sangu.

Pia aliwataka watanzania kusherehekea siku hiyo kwa amani, utulivu na kusaidia watu wenye uhitaji badala ya kufanya anasa na ulevi.

**KUTUNZA MUDA**

Msaidizi wa Askofu Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Usharika wa Azania Front, Dayosisi ya Mashariki na Pwani, Chediel Lwiza, aliwataka waumini wa kanisa hilo katika mwaka wa 2024, wautumie muda wao vizuri ili wayafikie malengo yao kwa kuwa muda ndio kila kitu.

"Mungu amewapa kibali cha kuona mwaka mwingine, maana yake amewapa muda tena wa kutengeneza maisha, hivyo utumie vizuri ili mpate baraka na maisha yenye tija kwenye familia zenu," alisema.

**MAADILI WATOTO**

Akizungumza katika ibada ya mkesha wa mwaka mpya, Mchungaji Kiongozi wa Kanisa la Efatha Zanzibar, Herry Nelson aliwataka wakulima katika mwaka mpya walime ili taifa liwe na chakula cha kutosha.

Pia aliwataka wazazi na walezi kuwalea watoto katika maadili mema na kuwalinda dhidi ya mitandao ya kijamii.

"Tuzitumie social media (mitandao ya kijamii) vizuri ili kujenga na kulinda maadili ya watanzania, watoto waangalie 'media' chanya ili wasipotoke," alionya.

Vilevile, kiongozi huyo alisisitiza umuhimu wa ibada kwenye ngazi ya familia na kuendeleza amani ya nchi.

**UONGO WANANDOA**

Paroko wa Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Dodoma, Michael Gaula aliwataka wanandoa kuacha kusema uongo kwenye familia zao ili kuepuka wimbi la talaka na ndoa kuvunjika linalotikisa nchi kwa sasa.

Alisema ndoa nyingi zimekuwa na migogoro kwa kuwa watu wameshindwa kusema ukweli kwenye familia zao.

Akihubiri katika ibada ya Mwaka Mpya kwenye Kanisa Katoliki la Paulo wa Msalaba Jimbo Kuu la Dodoma, Gaula alisema mojawapo ya sababu zinazochochea ndoa kuvunjika ni uongo.

Alisema wamekuwa wanapokea barua za kuomba talaka kwa wanandoa na wanapouliza chanzo, wanabaini wanandoa wengi hawasemi ukweli, wameendekeza uongo.

Kwa kutambua hilo, alisisitiza upendo ndani ya nyumba na kujenga utaratibu wa kusema ukweli katika ndoa.

"Tunaomba mjenge utaratibu wa kuwa wakweli, tunahitaji kuona ndoa zinadumu kwenye familia zenu," alisema.

Alisema jamii ikisema ukweli kwenye familia, ndoa nyingi zitadumu na kutapunguza tatizo la talaka.

Gaula alitaka jamii kuacha kusherekea mwaka kwa kutenda matendo mabaya, badala yake wawe mfano bora wa kuigwa katika kazi zao za kila siku.

Alisisitiza pia kuwaombea viongozi wa serikali ili waongoze vizuri katika maeneo mbalimbali nchini.

**UCHAGUZI S/MITAA**

Akitoa salamu za Mwaka Mpya, Mhadhiri Mwandamizi wa Chuo Kikuu cha SAUT Kampasi ya Mwanza, Prof. Eustad Tibategeza, alisema katika mwaka 2024 taifa linahitaji maombezi makubwa pamoja na neema ya Mungu ili kupita salama katika kipindi chote cha uchaguzi.

Akitoa salamu hizo katika misa takatifu ya mkesha wa Mwaka Mpya iliyofanyika Kanisa la Mtakatifu Martine De Pores lililoko chuoni huko, Prof. Tibategeza alisema watanzania wanapaswa kuombea Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu.

Padri wa kanisa hilo, Charles Bundu, akiongoza ibada hiyo aliwataka vijana kutunza ujana na utu wao kwa kuhakikisha wanatenda matendo yanayokubalika kwa Mungu na kuacha vitendo visivyofaa katika jamii.

"Kijana unatakiwa kuheshimu na kuthamini ujana wako wala usiwafanye watu waudharau ujana wako kwa namna yoyote, enenda katika mapenzi ya Mungu na yale yasiyofaa achana nayo kabisa," alihimiza.

**AMANI, UTULIVU**

Paroko Msaidizi wa Parokia ya Usagara, Theogene Nibogora wakati wa ibada ya kuuaga mwaka 2023 na kuukaribisha mwaka 2024, iliyofanyika katika Kanisa Katoliki la Mtakatifu Yohana Mwinjili Jimbo Kuu la Mwanza, alitaka watanzania waendelee kudumisha amani na utulivu.

Alisema upendo na amani iliyopo nchini inatakiwa kulindwa ipasavyo katika mwaka unaoanza bila kujali dini wala mahitaji ya itikadi yoyote ya vyama vya kisiasa.

**VIJANA NA UONGOZI**

Mkuu wa Kanisa la Pentekosti Christian International Tanzania, Askofu Thomas Kiula aliwataka vijana wenye sifa za uongozi kuchangamkia fomu za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa utakaofanyika mwaka huu badala ya kuendelea kuwa wapigadebe kwa wengine.

Alitoa rai hiyo wakati wa ibada ya kuukaribisha Mwaka Mpya iliyofanyika katika kanisa hilo.

Alisema vijana badala ya kuwa wapigadebe kwa watu wengine, nao wanatakiwa kujitokeza kwa wale wenye sifa ya kuwania uongozi.

"Ninawahamasisha mjitokeze kwa wale wenye uwezo na vigezo vya kuwa viongozi kwa mwaka huu. Ninawaomba mchangamkie msisubiri wengine wajitokeze na ninyi mkabakia kuwa madaraja ya kuwapitisha hata kama hawana vigezo vya kuwa viongozi.

"Kipenga cha Tume ya Taifa ya Uchaguzi kikipulizwa tu, vijana nendeni mkachukue fomu hizo za uchaguzi na sisi kama kanisa tutaomba kwa Mungu ili atupatie viongozi walio wake ambao wenye hofu na maadili ya kiroho," alihimiza.

Pia aliwataka watanzania kuhakikisha mwaka wa 2024 unakuwa kwa kila mtu kufanya kazi za kujiletea uchumi.

Alisema kuwa mwaka 2024 uwe wa mafanikio ya kujiimarisha zaidi kwa kufanya kazi za kiuchumi na kwenye kilimo badala ya kukaa vijiweni na wengine kusubiri kupatiwa misaada.

**MIKOPO UMIZA**

Mwenyekiti wa Parokia ya Kristo Mfufuka ya Kanisa Katoliki wilayani Muheza, Mary Kauki wakati wa ibada ya Mwaka Mpya iliyoendeshwa na Padri Martine Kihiyo, aliwasihi wanawake kuepuka kujiingiza katika mikopo ya kausha damu.

"Wanawake wenzangu tuachane na mikopo chechefu ya kausha damu ambayo inatusababishia kuuza vitu vya ndani mpaka nguo," alisema Mary.

Alisema kuwa wanawake wengi katika kanisa hilo wameingia katika mikopo hiyo ya kausha damu, wanashindwa hata kulipa ada za jumuiya za kanisani.

Alisema waumini wanapenda kujiingizia katika vikundi vya kukopa vya kausha damu ambayo si vizuri. Ni aibu kwa waumini hao.

Padri Kihiyo alihimiza upendo miongoni mwa watanzania wanapoingia katika mwaka mwingine.

Mchungaji wa Kanisa na Kiinjili la Kirutheri Tanzania (KKKT) Usharika wa Muheza Mjini, John Ndimbo aliwahimiza watanzania kuwaombea viongozi.

***Imeandaliwa na Steven William (Muheza), Marco Maduhu (Shinyanga), Jenipher Gilla (Dar), Rahma Sileiman (Zanzibar), Renatha Msungu (Dodoma), Vitus Audax (Mwanza), Peter Mkwavila (Dodoma).**

HABARI KITAIFA

# NMB yawajaza mamilioni wafanyabiashara wa soko lililokumbwa na mafuriko Mwanza

**Na Mwandishi Wetu,**
MWANZA

WAFANYABIASHARA 15 wa soko la Mlango Mmoja, wilayani Nyamagana, mkoani Mwanza wamenufaika na bima ya Sh. milioni 36.5 kutoka kwa Benki ya NMB pamoja na kampuni ya bima ya Reliance Tanzania Ltd.

Wafanyabiashara hao wamelipwa fedha hizo baada ya soko hilo kupata majanga ya mafuriko Desemba 10, mwaka huu.

Akizungumza juzi wakati wa hafla ya kukabidhi malipo ya fidia ya bima katika soko la machinga la Mlango Mmoja, mmoja ya wanufaika wa bima ya NMB, Levina Derick alishukuru benki hiyo kwa kuwapatia fedha hizo.

Alisema bima zinasaidia, hivyo bila bima ya NMB, asingeweza tena kupata mtaji wake. Alisema mtaji wake wa nguo za mtumba ulisombwa na mafuriko.

Katibu wa soko la Mlango Mmoja, Siriacus Rwezaura aliomba Benki ya NMB iongeze elimu kuhusu bima ili wafanyabiashara wengi katika soko hilo wakatiwe bima.

"Soko letu la Mlango Mmoja lina wafanyabiashara 1,000, lakini waliokata bima ya biashara ni 15 tu, elimu ya bima inahitajika sana," alisema.

Mwakilishi wa Kitengo cha Bima, Benki ya NMB makao makuu, Adam Msenga alisema benki hiyo NMB itaendelea kubuni bidhaa mbalimbali kwa ajili ya wafanyabiashara, makondakta na mama lishe.

Alisema Benki ya NMB imefanikiwa kulipa madai ya wafanyabiashara 15 waliopata majanga ya mafuriko. Aliwaomba wafanyabiashara wa soko hilo kutumia huduma ya NMB mkononi.

"Benki yetu ina bima za bei nafuu sana, mfanyabiashara anaweza kulipia bima ya kuanzia Sh. 10,000 kwa mtaji wa Sh. 500,000 na Sh. 60,000 kwa mtaji wa Sh. milioni 10," alisema.

Meneja wa Kampuni ya Bima ya Reliance Limited, Joel Mwakalebela alisema kampuni yao kwa kushirikiana na Benki ya NMB wamekuja na suluhisho la 'bima ya machinga' kwa lengo la kusaidia wafanyabiashara wakati wa majanga.

Mwakilishi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA), Khalfan Jumanne alisema mamlaka yao ina kazi ya kusimamia soko la bima.

Alishauri wafanyabiashara kuhakikisha wanakata bima katika Benki ya NMB kwa lengo la kulinda mali zao.

Aliishukuru benki hiyo na kampuni ya bima ya Reliance kwa kuwasaidia wafanyabiashara wa Mlango Mmoja.



# TRA yaandika rekodi nyingine ya makusanyo

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) imetangaza makusanyo ya mapato katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2023/24 (Julai hadi Desemba 2023), yakipanda kwa asilimia 11.5 kulinganishwa na mwaka 2022/23.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Kamishna Mkuu wa TRA, Alphayo Kidata, katika kipindi hicho cha nusu mwaka imekusanya Sh. trilioni 13.92, ambayo ni sawa na ufanisi wa asilimia 97.98 ya lengo la kukusanya Sh. trilioni 14.21.

"Makusanyo haya ya nusu mwaka ni ongezeko la asilimia 11.5 kulinganishwa na makusanyo ya Sh. trilioni 12.49 yaliyofikiwa katika kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha uliopita, 2022/23," alisema.

Alieleza zaidi kwenye taarifa hiyo kuwa katika kipindi cha mwezi Desemba 2023, TRA iliandika rekodi mpya ya kiwango cha juu cha makusanyo kwa mwezi tangu kuanzishwa kwake kwa kukusanya Sh. trilioni 3.05, ikiwa ni ufanisi wa asilimia 102.99 ya lengo la kukusanya Sh. trilioni 2.96.

Makusanyo hayo ni ongezeko la asilimia 9.2 kulinganisha na kiasi cha Sh. trilioni 2.79 kilichokusanywa katika mwezi kama huu katika mwaka wa fedha 2022/23," TRA ilifafanua.

Alisema mafanikio hayo yaliyofikiwa katika nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2023/24 yamechagizwa na juhudi za mamlaka katika kutekeleza kwa vitendo maelekezo na miongozo mbalimbali inayotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan pamoja na viongozi wengine wa serikali katika ngazi mbalimbali.

Vilevile, alisema TRA imeendelea na utekelezaji wa Mpango Mkakati wake wa Sita (CP6) wenye athari chanya katika ukusanyaji wa mapato nchini ambapo miongoni mwa hatua zilizochukuliwa ni pamoja na maboresho katika muundo wa TRA ikiwamo uanzishwaji wa divisheni mpya za walipakodi wa kati na walipakodi wadogo ili kutoa huduma bora na stahiki kwa makundi tofauti ya walipakodi kwa kuzingatia utofauti wa mahitaji yao.

"Katika kuendeleza mafanikio hayo, TRA inatoa wito kwa walipakodi na umma kwa ujumla kuendelea kutekeleza matakwa ya sheria za kodi kwa hiari ikiwamo kuwasilisha ritani na kulipa kodi stahiki kwa wakati, kutoa na kudai risiti za kielektroniki (EFD) kwa kila ununuzi wa bidhaa au huduma unaofanywa, kuendelea na uhakiki wa stempu za kielektroniki za kodi (ETS) kabla ya ununuzi na matumizi ya bidhaa, na kutoa taarifa za viashiria vya upotevu wa mapato ya serikali.

"Jitihada hizi za pamoja zitasaidia kufikia lengo la mwaka wa fedha 2023/24 la kukusanya jumla ya Sh. trilioni 28.35 na hivyo kuiwezesha serikali kutoa huduma bora kwa wananchi na kutekeleza mipango ya maendeleo kwa ustawi wa taifa letu," Kidata alisisitiza katika taarifa yake hiyo.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya BUGANDO**
**Wilaya ya GEITA**
**Mkoa ............................ GEITA**
**Shauri la TALAKA Na 30/2023**
**Jina la Mdai: MICHAEL MABULA**
**Jina la Mdaiwa: SOFIA NYERERE**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuniya 18 ya kanun iza taratibu Madai katika mahakama za Mwanzo)**

**Kwa:SOFIA NYERERE**
**WA NKOME**

**AMRI: -** Unaamriwa na Jamuhuri uhudhurie Mahakamani hapa siku ya Alhamisi tarehe 4/1/2024 saa 2:00 Asubuhi ili ujibu madai ya Talaka. Usipohudhuria kesi itasikilizwa bila wewe kuwepo
Unaonywa usikose kuhudhuria.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo Tarehe 19 Mwezi 12 Mwaka 2023

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
BUGANDO
..........................................
**HAKIMU**





The Management and Staff of The Guardian Limited
wish you a successful New Year 2024.
We are very grateful for having you as our
business partner.
Thank you for your valuable patronage.
Your trust is highly appreciated.

Subscribe today our News Paper
epaper.ippmedia.com

IPPmedia The Guardian Nipashe

NipasheTz @TheguardianTz01 theguardianltd epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com +255 745 700 710

# Dk. Mwinyi aipongeza NMB kuunga mkono ajenda maendeleo endelevu

**Na Mwandishi WETU,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi amepongeza Benki ya NMB kwa kuendelea kuunga mkono ajenda ya maendeleo endelevu visiwani Zanzibar.

Akizungumza baada ya kushiriki katika matembezi ya sherehe za miaka 60 ya Mapinduzi Zanzibar yaliyofanyika mjini Zanzibar, Dk. Mwinyi alipongeza benki hiyo, akibainisha kuwa msaada wake umekuwa chachu katika kukuza uchumi na kuleta maendeleo endelevu visiwani hapa.

"Benki ya NMB imekuwa inashirikiana kwa karibu na serikali yetu katika kuchochea maendeleo ya sekta mbalimbali za Zanzibar.

"Ninatumia fursa hii kuipongeza Benki ya NMB kwa kuendelea kutuunga mkono na ningependa kuchukua fursa hii kuyaomba mashirika mengine yanayofanya kazi visiwani hapa kuunga mkono ajenda yetu ya maendeleo," alisisitiza Dk. Mwinyi.

Awali Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo Zanzibar, Tabia Maulid Mwita pia aliimwagia sifa benki hiyo na kuongeza kuwa imekuwa na mchango mkubwa katika kukuza maendeleo ya sekta ya michezo visiwani Zanzibar.

Mwita alishukuru benki hiyo kwa kushiriki kikamilifu katika matembezi ya sherehe za miaka 60 ya Mapinduzi Zanzibar baada ya benki hiyo kutoa udhamini wa Sh. milioni 200 wa vifaa vya michezo hivi karibuni.

Alisisitiza dhamira ya wizara kuendelea kushirikiana na wadau mbalimbali wa Zanzibar ili kuimarisha maendeleo ya michezo.

Meneja wa Biashara ya Zanzibar wa Benki ya NMB, Naima Said Shaame wakati wa hafla hiyo alisisitiza dhamira ya benki hiyo kuendelea kufanya kazi kwa karibu na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kuongeza kuwa mbali na kusaidia miradi mbalimbali ya maendeleo, benki yao imekuwa na mchango mkubwa katika uwekezaji wa kijamii ikiwa ni sehemu ya dhamira yake ya kukuza thamani ya wadau wake wote ikiwa ni pamoja na jamii ambako benki inafanyia kazi.

"Sisi kama benki, tutaendelea kuunga mkono kikamilifu utekelezaji Ajenda ya Uchumi wa Bluu ya Serikali ya Zanzibar kupitia utoaji huduma bora za kibenki ninazokidhi matakwa ya wateja wetu," alisema.




Masta Shangwe (mwenye kofia ngumu) pamoja na Meneja wa Vodacom Tanzania Kanda ya Kaskazini, George Venanty (wa kwanza kushoto) wakikabidhi mfano wa kadi ya bima kwa Muuguzi Mfawidhi Simphorosa Silalye (wa kwanza kulia) na mmoja wa kinamama walionufaika katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Arusha (Mt. Meru) mwishoni mwa wiki. Kupitia kampeni yake inayoendelea ya 'Sambaza Shangwe, Gusa Maisha', kampuni hiyo imekabidhi kadi za bima kwa kinamama 100 na watoto 100 hospitalini huko ikiwa ni zawadi ya upendo msimu huu wa sikukuu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# ACT yataka uchunguzi vifo vya vijana wawili Dar

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha ACT Wazalendo kimesema kimepokea kwa masikitiko taarifa ya maofisa wa Jeshi la Polisi kuhusishwa na vifo vya vijana wawili; Bakari Ismail (21) na Shomari Kucheuka (22) waliokuwa wanaishi Vingunguti, Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Jeshi la Polisi mwishoni mwa wiki, vijana hao walifariki dunia baada ya kupigwa risasi miguuni na askari polisi waliokuwa wanakabiliana nao wakiwa na silaha za jadi.

Hata hivyo, katika taarifa yake kwa vyombo vya habari juzi, Wakili Bonifasia Mapunda, Waziri Kivuli wa Mambo ya Ndani wa ACT Wazalendo, alidai kuwa vijana hao walikamatwa kwa nguvu na askari polisi wakiwa nyumbani kwao mnamo Desemba 27, mwaka jana.

"Jambo la kusikitisha baada ya kukamatwa haikujulikana walipelekwa wapi kwa kuwa jitihada za ndugu na jamaa kufuatilia kwenye vituo vya polisi takriban siku sita hazikufanikiwa kuwapata vijana hao.

"Vilevile, hawakuweza kuwapata kwenye hospitali hadi ilipofika tarehe 28 Desemba walipotaarifiwa kuwa miili ya vijana hao iko Hospitali ya Amana iliyofikishwa na askari polisi," alidai.

Wakili Bonifasia alisema ACT Wazalendo inaona zipo hoja zinazoonesha kuhusika kwa Jeshi la Polisi kwenye mauaji hayo.

"Mosi, kutajwa kwa askari polisi wakati wa ukamataji na baadaye tena kwenye kufikishwa miili ya vijana hao katika Hospitali ya Amana.

"Pili, si kawaida ya Jeshi la Polisi kuokota miili ya watu halafu ikaipeleka hospitalini wakati tayari kuna taarifa ya watu walioulizia kuhusu ndugu zao," alisema.

"Kutokana na kujirudia kwa matukio na tuhuma za askari polisi kuhusishwa kwenye mauaji, ni wazi taswira ya Jeshi la Polisi inaendelea kuchafuka na kushusha imani ya wananchi.

"ACT Wazalendo tunarudia wito kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania liunde tume ya kuchunguza mauaji yote ya raia ili kujiridhisha na hatua zilizofanywa na Jeshi la Polisi.

"Pili, kwa hatua za awali tunamtaka Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam kuchukua hatua ya kufuatilia wanaotajwa kuhusika kwenye tukio hili la vijana," alisema.

Waziri kivuli huyo pia alisema wanaendelea kusisitiza mageuzi ya Jeshi la Polisi kutoka kuwa alichokiita chombo cha mabavu na kuwa huduma ili liwe linatekeleza wajibu na majukumu yake kwa weledi na kufuata sheria.

# Anamringi: Mpasuko wa viongozi bado tatizo CCM

**Na Romana Mallya**

KAIMU Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Anamringi Macha amesema moja ya mambo waliyonayo ndani ya chama ni mpasuko wa viongozi, akisisitiza kuwa wananchi na wanachama hawana shida.

Ameeleza kuwa kitu kinachomtesa, kumwumiza na kumchosha Mwenyekiti wa CCM, Rais Samia Suluhu Hassan, ni aliowateua katika chama na serikali, badala ya kuwa wamoja na kufanya kazi, wanafarakana.

Aliyasema hayo juzi mkoani Dar es Salaam wakati wa mkutano mkuu maalum ulioandaliwa na Jimbo la Ubungo chini ya Mbunge wake, Prof. Kitila Mkumbo, kwa lengo la kutoa taarifa ya utekelezaji Ilani ya CCM ya 2020/2025.

Alisema kutokana na kuwapo hali hiyo, watakuwa wanamshauri Rais Samia awaondoe viongozi wanaoendekeza makundi ili wabaki na viongozi wanaofanya kazi.

Anamringi ambaye pia ni Naibu Katibu Mkuu wa CCM Tanzania Bara, alisema, "wenye shida ni sisi, lakini hakuna kitu kinacholeta ladha kubwa kama unaposikia mbunge anasema mwenyekiti wangu, mwenyekiti anasema, katibu wangu, mbunge anasema DC (Mkuu wa Wilaya).

"Hilo ni jambo tunatakiwa tulitunze. Mbunge anasema madiwani wangu, yapo maeneo ambayo mbunge hasemi madiwani wangu, lakini tukitaka kuchukua hesabu za kweli, mbunge ni kiranja mkuu kwa madiwani na madiwani wanakubali kuwa viranja," alisema.

Hivyo, alimpongeza Mbunge wa Ubungo, Prof. Mkumbo, ambaye jimboni kwake alikiri madiwani wapo pamoja naye.

Aliwaeleza kuwa wanamchosha sana Mwenyekiti Samia wanapoparanganyika ngazi ya chini.

**WANAOJIPITISHA MAJIMBONI**

Anamringi pia aliwakumbusha wana CCM kuwa bado miaka miwili ya kuingia katika uchaguzi mkuu na kuna kazi zinaendelea kufanyika.

Alisema si sahihi wakajitokeza watu kuanza kufikiria ubunge au udiwani nje ya wakati wake.

Alisema wale wote wanaojaribu kuvunja utaratibu wa kutafuta uongozi, waendelee lakini ifikapo Septemba 2025, watajuta watawekwa pembeni.

"Unasikia mfano Ubungo kuna mbuzi cup, ng'ombe cup au kobe cup, subirini mechi za Simba na Yanga, unaanzisha mechi mtaani, tuachane na hizo cups (vikombe) za uongo. Tafuta pikipiki au baiskeli ulete ofisi ya chama," alionya.

Akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya CCM jimboni Ubungo, Prof. Kitila alisema wamefanikiwa kupiga hatua katika sekta tofauti.

Alisema uanzishwaji tuzo kwa walimu ambayo huhusisha kutambua mchango wa walimu kwa wanafunzi wanaofaulu somo la Hisabati, umewezesha kuinua ufaulu.

Alisema takwimu zinaonesha mwaka 2020 kabla ya kuanzishwa tuzo hizo, ufaulu somo la Hisabati kwa alama A hawakuwapo na alama B walikuwa tisa.

"Mwaka 2021 ufaulu wa alama A walikuwa 30 na alama B walikuwa 31. Mwaka 2022 alama A waliongezeka na kufikia 48 na alama B walikuwa 39," alisema.

Pia alisema mwaka 2020 upungufu wa vyumba vya madarasa ulikuwa kwa asilimia 23 na mwaka 2023 umepungua hadi asilimia 1.2.

Alisema kwa upande wa matundu ya vyoo, mwaka 2020 upungufu ulikuwa kwa asilimia 60 na sasa umepungua hadi asilimia 48; madawati upungufu ulikuwa kwa asilimia 34 na sasa umepungua na kufikia asilimia nne na upungufu wa ofisi za walimu ulikuwa ni asilimia 63 na sasa umepungua hadi asilimia 38.

Kuhusu miundombinu, alisema kupitia mradi wa DMDP, Ubungo imeidhinishiwa kilometa 24.56 za barabara zitakazojengwa kwa kiwango cha lami kwa Sh. bilioni 42.980.

Pia alisema Mfuko wa Jimbo utatoa Sh. milioni 20 kwa ajili ya ujenzi wa kivuko cha Ubungo Kisiwani na Sh. milioni 10 kwa kivuko cha Usewe.

HABARI KITAIFA

# TMA yatoa tahadhari mvua kubwa katika mikoa mitano

**Na Jenifer Gilla**

MAMLAKA ya Hali ya Hewa nchini (TMA) imetoa tahadhari ya kunyesha mvua kubwa katika baadhi ya maeneo ya mikoa ya Pwani (hasa visiwa vya Mafia), Dar es Salaam, Morogoro, Lindi na Mtwara.

Imesema mvua hiyo inaweza kusababisha athari ikiwamo mafuriko, baadhi ya maeneo kuzungukwa na maji na kuharibu shughuli za kiuchumi. Kutokana na hali hiyo, TMA imewakumbusha wananchi kuchukua tahadhari na kujiandaa kwa mvua hiyo ikiwamo kununua mahitaji yao ya msingi na kuyaweka ndani ili kuepuka kutembea wakati mvua inanyesha.

Dar es Salaam ni moja ya mikoa ambayo mvua kubwa ikinyesha kunatokea mafuriko yanayosababishwa na mambo mengi ikiwamo mitaro inayopitisha maji kuziba.

Hali hiyo imekuwa inaleta usumbufu kwa wakazi wa jiji hilo hasa wale wanaoishi pembezoni mwa mito, nyumba zimekuwa zinasombwa na maji, usafiri umekuwa shida na foleni za magari kuwa kubwa na maeneo mengine yamekuwa yanazingirwa na maji na kusababisha kupitika kwa shida.

Julai 29, mwaka huu, TMA ilitangaza ujio wa El Nino katika kipindi cha msimu wa vuli. Mvua ilitarajiwa kuanza kunyesha mwezi Oktoba hadi Desemba, mwaka huu, kukiwa na angalizo kwamba inaweza kusababisha athari katika maeneo mbalimbali nchini.

TMA ilieleza kuwa mvua hiyo inaweza kuleta madhara kwa binadamu na mazingira ikiwamo vifo, mafuriko, maporomoko ya ardhi, upotevu mali, magonjwa ya mlipuko na uharibifu wa miundombinu hivyo kuwataka wananchi kuchukua tahadhari.

Katika kukabiliana na changamoto hiyo, Oktoba 13 mwaka huu, Ofisi ya Waziri Mkuu ilizindua Mpango wa Taifa wa Dharura wa Kuzuia na Kukabiliana na Madhara ya El-Nino na kuugawa kwa viongozi wakuu wa serikali, wakiwamo mawaziri, naibu mawaziri, makatibu wakuu na taasisi za serikali kwa ajili ya kuanza utekelezaji wake.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, pamoja na mambo mengine, wakati wa uzinduzi wa mpango huo, alielekeza TMA kuandaa mfumo mzuri wa kutoa taarifa kuhusu mwenendo wa mvua hiyo kwa wananchi kupitia ujumbe mfupi wa simu.

Mvua hiyo tayari imeshasababisha madhara mbalimbali nchini, vikiwamo vifo, tukio kubwa zaidi likiwa la maporomoko ya tope, mawe na magogo toka Mlima Hanang yaliyosabanisha vifo vya watu 89 na kuharibu makazi na miongombinu mingine wilayani Hanang, mkoani Manyara.

## Mjamzito afariki dunia akidaiwa kunyimwa huduma hospitalini

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

RACHEL William (19), mkazi wa mtaa wa Mji Mwema, wilayani Kahama, mkoani Shinyanga, amefariki dunia baada ya kudaiwa kunyimwa huduma ya kujifungua katika Hospitali ya Halmashauri ya Manispaa ya Kahama.

Tukio hilo lilitokea Desemba 27, mwaka jana saa nane usiku wakati Rachel alipofika hospitalini huko kujifungua, lakini hakujifungua kwa wakati kwa kile kinachodaiwa kunyimwa huduma na mtoahuduma aliyetaka rushwa.

Akizungumza na Nipashe kuhusu tukio hilo, msemaji wa familia, Mwanambala Shinje alidai kuwa Rachel alifika katika hospitali hiyo, akitokwa na damu sehemu za siri.

Alidai kuwa mtoahuduma wa zamu (jina limehifadhiwa) alishindwa kumpa huduma kwa haraka kwa kile kinachoelezwa akidai kupewa fedha, hali ambayo baadaye ilisababisha umauti kwa Rachel saa 6:30 mchana.

Msemaji huo alidai kuwa ndugu yao alipelekwa usiku huo Hospitali ya Manispaa ya Kahama, lakini muda huo alikosa huduma kwa kuombwa rushwa ya kiasi ambacho hakukitaja.

Alidai kuwa daktari wa zamu siku hiyo ndiye aliyewataka kutoa fedha ili wapatiwe huduma huku akitoa lugha isiyo ya kiungwana kwa madai kuwa hawezi kuingiliwa kwenye kazi yake, akitumia lugha ya Kiingereza zaidi, huku akiendelea kuchati kwa simu ya mkononi.

Alidai baada ya kifo cha Rachel alileletwa muhtasari ili kusaini na kuchukua mwili kwenda kuzika, lakini mtuhumiwa wa tukio hilo, hakuandika jina na hata alipotaka kuonana na mtuhumiwa huyo ilishindikana, hivyo wakaamua kuacha mwili huo.

Msemaji wa familia alidai kuwa baadaye alikubali kuchukua mwili wa marehemu na kwenda kuuzika baada ya kushauriana na uongozi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, akiahidiwa wahusika kuchukuliwa hatua za kinidhamu.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Clemence Mkusa alithibitisha kutokea uzembe wa madaktari na wauguzi wa zamu siku hiyo. Hatua za kinidhamu zimeanza kuchukuliwa dhidi yao kwa kutakiwa kuandika maelezo ya kujieleza ili yafikishwe kwenye kamati ya maadili ya hospitali kwa hatua zaidi. Pia alisema wameshirikisha na Jeshi la Polisi wilayani hapa kwa ajili ya upelelezi wa tukio hilo ili kubaini wahusika.

Mbunge wa Ushetu, Emmanuel Cherehani alisema watoto na kinamama, hasa wajawazito, wanateseka kupata matibabu wanapofika hospitalini.

Alisema wengi wanapoteza maisha kwa kukataa kutoa rushwa ambazo wanaombwa na madaktari na wauguzi wasiokuwa na maadili ya kazi. Alitaka wahusika wa tukio hilo wachukuliwe hatua.

Akitolea mfano, alisema katika Kata ya Chambo, kuna mama alipoteza kichanga chake baada ya kushindwa kutoa rushwa ya Sh.150,000 aliyoombwa na madaktari wa Kituo cha Afya Ukune.

Alisema walifanya ukaguzi hadi wahusika wakapatikana na baadhi yao walifukuzwa kazi.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Shinyanga, Mabala Mlolwa alidai taarifa ya kifo hicho zimeshamfikia Rais Samia Suluhu Hassan na amemwagiza kuleta salamu za rambirambi na kuahidi wahusika wote kuchukuliwa hatua za kinidhamu.



# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## *Kunahitajika hatua zaidi, marufuku ya dawa bila cheti kwenye famasia*

**KATIKA** nadharia ya jumla kisomi, matumizi ya dawa na hata aina za huduma za kitabibu, daima zinahimiza nyendo zote husika zinaangukia kwenye mwongozo wa daktari husika.

Pia daktari husika mbali na uelewa wake kitaaluma unaokubalika, utendaji wake nao unaongozwa na kanuni zake kikazi, sambamba na zile za afya kitaifa.

Kimsingi, iko hata katika kanuni za afya zinazotumika kitaifa chini ya Wizara ya Afya, nazo ziko chini ya Shirika la Afya Duniani (WHO).

Eneo moja ambalo utelekezaji wake hauhitaji mjadala ni katika matumizi ya dawa, kigezo na masharti ni kwa mtumiaji afanye hivyo kwa maelekezo rasmi ya daktari anayemtibu au kumsimamia. Hiyo inatajwa kuwa na faida kwa wote, zaidi anayetibiwa ugonjwa, hali kadhalika wanaofanikisha tiba hiyo kufikiwa, kuanzia daktari, manesi na watoa dawa.

Kadri siku zinavyosonga, kunaonekana kuwapo udhaifu kwamba wagonjwa mbalimbali wanaenda kufuata dawa katika maduka, kwa sababu kama za kujitibu wakihisi wanajua zaidi, wanabana matumizi ya pesa au kutokuwa na fedha za kumuona daktari.

Hospitalini kuna madaktari wanaofanya kazi za kuwasikiliza na kisha kuwashauri dawa wagonjwa, wakitumia nyenzo kama za maabara, ndio mgonjwa anashauri dawa ya kuuziwa.

Nje ya hapo, kuna hatari mgonjwa kuangukia pabaya, anaumia huku serikali nayo inabeba mzigo wa wanaougua kitaifa.

Serikali baada ya kugundua hilo imeamua kuchukua hatua kali, ikiwamo kupiga marufuku utoaji dawa hizo kiholela, nafasi hiyo ikirejeshwa kwa madaktari walioko katika maeneo rasmi ya kitabibu kama zahanati na hospitali.

Katika usemi 'sasa inatosha' mwaka 2021, serikali kupitia Wizara ya Afya ambako kuna Msajili wa Baraza la Famasia, Elizabeth Shekalaghe, akatamka marufuku hiyo akitoa ufafanuzi kwamba mahali hapo siyo hospitali, penye jukumu la kuelekeza utabibu.

Msajili akafafanua kwamba, maduka ya dawa hayana idhini ya kutoa matangazo ya kufanya ushauri wa kitabibu, akienda mbali kwa kutaka ushirikiano wa umma, unapobaini duka la dawa linakiuka, pia inaendeshwa pasipo kuwa na vibali maalum, ziripotiwe kwa mamlaka husika.

Kimajukumu, Baraza la Taifa Famasia ni taasisi ya serikali chini ya Wizara ya Afya chini ya Sheria ya Famasi, ikiwa na jukumu la kusimamia dawa, ikiwamo usajili wa wanataaluma wa fani yake.

Ni neno linalotiliwa mkazo mara nyingi na serikali. Mwaka 2018 ikitamka marufuku ya mtu kwenda kununua dawa bila ya kuwa na cheti cha kitabibu, kisha na miaka mitatu baadaye, 2021 ikarudia tena kwa tamko la Msajili.


Hilo ndilo katika mwisho wa mwaka ulioishia wikiendi iliyopita, tukasikia tena marufuku hiyo kwenye vyombo vya habari 'hakuna kununua dawa pasipo cheti.'

Ikifuatiliwa kwa kina, kuna hesabu ya wastani wa kila miaka mitatu, serikali inapaza sauti kwa umma kuwa makini katika matumizi ya dawa bila ya vyeti au ushauri wa kidaktari.

Hapo ndipo sisi Nipashe tunaungana kupaza sauti hiyo ya kitaalamu na kiafya kutoka serikalini kwamba mwenye dhamana anapopaza sauti, kuna maana kubwa ya kuwapo walakini sugu umetawala. Vilevile ni kelele inayopaswa kuheshimiwa, maana inalenga kutetea afya ya Mtanzania anayeumwa au kuhisi kuugua na wakati huohuo ina misingi ya kulinda maslahi ya umma, katika tafsiri pana ya maisha.

Umefika wakati muafaka wa umma kubadilika kufuata suati inayopazwa, huku serikali nayo isonge kwa hatua zaidi mkono wa sheria na agizo la nidhamu zichukuliwe, katika utii wa matumizi ya dawa, kwa tafsiri pana inayofika ndani, gharama za kiserikali zitokanazo na watu wengi kuugua na gharama, katika kile kinachodhibitika.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

Na Mwandishi Wetu

# *Heri ya mwaka mpya pole na kero za usafiri*

**KILA** uchao, kumekuwa kukiibuka kero mpya kibao kwa abiria wanaotumia usafiri wa daladala jijini Dar es Salaam na hata kwingineko mikoani.

Kwa mwaka 2023 ambao tumeumaliza hivi punde hadi sasa kumekuwepo kero kwa baadhi ya daladala kukatisha ruti kwa visingizio, ikiwemo ubovu wa barabara au tamaa ya kupata fedha zaidi ya ile nauli ambayo imepangwa na serikali.

Visingizio vingine ni baadhi ya madereva kukiuka sheria zilizowekwa na serikali na ubovu wa vyombo hivyo vya usafiri.

Kuna kero ambazo zimeendelea kuota mizizi kwa baadhi ya daladala zinazoteremsha abiria karibu robo tatu ya waliokuwa wakisafiri kabla ya kufika mwisho wa safari kufaulishia waliosalia kwenye daladala nyingine kwa makubaliano ya makondakta wa chombo kimoja kwenda kingine.

Mchezo huo ambao kwa wafanyakazi hao wa daladala umekuwa kama umehalalishwa kwa kuwalazimisha abiria kuteremka kwenye daladala moja kwenda jingine baada ya wao kukubaliana kulipia angalau kiasi fulani cha pesa kama kupoozana na kuwa kero kwa abiria husika.

Ni kero kwa sababu kinamuweka abiria huyo katika hali ya kuwa katika taharuki na kukosa amani kutokana na kulazimishwa kuteremka kwenye daladala kinyume na matarajio yake, kusimama badala ya kukaa kwenye siti kama alivyoanza safari yake katika daladala la awali akiwa katika hali ya uchovu.

Siyo siri wengi wa abiria wanaotumia usafiri wa daladala, mwanzo wa safari unaweza kuwa mgumu kutokana na 'mabavu' yanayotumika wakati wa kupanda ili kupata siti ya kukaa.

Abiria anapokaa kwenye siti, ndipo anapata utulivu kwa sababu anapata wasaa wa kupumzika huku baadhi yao wakiuchapa usingizi kutokana na uchomvu wa mihangaiko yao wakati wakujitafutia riziki iwe katika biashara au maofisi.

Abiria wengine wanatumia muda huo kusoma magazeti, kusikiliza muziki, kufuatilia matukio mbalimbali yanayotokea nchini na duniani kote, kuchati na kuperuzi katika simu zao za kupangusa (smartphone).

Ghafla kondakta anasikika akisema:" gari inaishia hapa, haya nyie mliopo teremkeni pandeni kwenye gari hii inafika hadi mwisho, hatuwezi kupoteza mafuta kwa watu wachache kama ninyi.

Abiria hao, pamoja na kubisha, kulalamika na kugomea amri ya kondakta, baadaye dereva anazima gari akimaanisha kuwa hafiki mwisho wa safari, hivyo watu wanalazimika kutii amri hiyo na kuteremka kisha kupanda kwenye daladala jingine wakiwa wamesimama.

Hapo abiria huyo atasafiri bila ya kuwa na tiketi jambo ambalo ni hatari endapo itatokea ajali kwani atakosa haki zake kwa kutokuwa na kielelezo. Kero nyingine kwenye daladala ni kuendelea kutumika kwa lugha chafu dhidi ya abiria toka kwa madereva na kondakta dhidi ya wanaosimama basi linapofurika watu asubuhi na jioni.

Daladala zinapokuwa na abiria wachache, makondakta wanatumia lugha za kuwabembeleza kwenye vituo zinaposimama wapande, zinapojaza inakuwa karaha kwao.

Kondakta atasikika akiwapanga abiria tena bila ya kujali umri wao kwa kumtaja jinsi alivyo bila kujali umri, we simama hivi, geukia kule shikilia bomba, acha kushika kiti utang'oa mara teremka kama sivyo.

Aidha, nyingine ambayo ni janga kubwa, ni baada ya kupandisha nauli za daladala kuanzia Shilingi 700 kutegemeana na umbali kama abiria hana nauli kamili, kondakta atakusanya fedha zake huku akitangaza hadi atakapopata chenji ndipo atamrudishia bila kujali kituo anapoteremkia na kuzua mizozo isiyo ya lazima ndani ya daladala.

Kero nyingine mbaya ni pale mvua zinaponyesha daladala zinavuja maji kutoka kwenye maeneo ya bodi ya juu yaliyooza na kwenye mipira ya kwenye madirisha iliyoisha na kusababisha baadhi ya abiria kulowana.

Kero hizo zinaweza kwisha kwa mwaka huu mpya wa 2024 iwapo mamlaka za usimamizi wa usafiri kama LATRA, Trafiki Polisi, Viwango TBS na vyombo vya sheria zitafanya ukaguzi wa mara kwa mara.

Kukagua usafiri na kuwabana wamiliki, makondakta na madereva kumjali mteja kwa kuwa ndiye mfalme kwenye kazi hiyo.

# Kinana: Wananchi wapewe nafasi kuamua masuala ya maendeleo yao

**Na Mwandishi Wetu,** LINDI

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Abdulrahman Kinana amesema umefika wakati mambo ya msingi yanayohusu maendeleo ya wananchi, lazima yaamuliwe na yatokane na wananchi wenyewe.

Amesema japokuwa wapo wawakilishi wa wananchi wakiwamo wabunge, madiwani au halmashauri, hawana uwezo wa kubadilisha hali iliyopo, hivyo ni muhimu wananchi wakapata nguvu zaidi kushiriki kuamua mambo ya muhimu kwao.

Kinana alitoa ushauri huo jana alipozungumza na wanachama wa CCM na wananchi wa Jimbo la Mtama, mkoani Lindi baada ya kuzindua Shina la chama huko Majengo Sokoni.

Akielezea zaidi kuhusu umuhimu wa wananchi kushirikishwa katika kuamua maendeleo, Kinana alitoa mfano kuwa kuna wakati akiwa Katibu Mkuu wa CCM, akiwa na Nape Nnauye, walikwenda wilayani Ngorongoro wakafanya mkutano mkubwa.

"Tulipokuwa pale, ukitazama pale, mimi ungeniuliza ningesema wale wananchi wanahitaji maji, lakini tulipouliza wenyeji wakasema tatizo lao si maji, bali ni mtandao wa simu.

"Unaweza ukaona wewe unakwenda mahali ukifikiri shida ya watu ni shule, ni maji kumbe shida yao ni jambo lingine kabisa, ndio! Ni lazima tuwashirikishe wananchi katika kuamua mambo yanayohusu maisha yao.

"Tusichukue amana ya kuwafikiria, tusichukue mamlaka ya kuwaamulia. Ni vizuri tukae na wananchi tuzungumze nao ili watuambie kitu gani wanakihitaji kwa wakati gani na kwa sababu gani," alisema Kinana.

Alifafanua kuwa ukiwaambia wananchi leo wajitolee kujenga barabara, wanaweza kukwambia wao wanataka shule kwanza huku akieleza katika mkutano huo kulitolewa hoja kuhusu kupeleka madaraka kwa wananchi.

"Kwahiyo, uundwaji wa vijiji, vitongoji, ni muhimu kwa maendeleo ya wananchi. Ukiangalia nchi yetu ilivyokaa wakati wa Uhuru katika miaka ya 1960 na 1970 tulikuwa na mikoa tisa, leo tuna mikoa zaidi ya 30. Tulikuwa na wilaya 50, leo tunakaribia wilaya 200 , tulikuwa na kata chache leo tunakata nyingi.

"Kwahiyo, Mwenyekiti na Mbunge nimewasikia kuhusu madaraka kwa wananchi. Tupeleke uamuzi kwa wananchi uwe na tija, lazima kuwe na taasisi inayosaidia wananchi kufanya uamuzi huo.

"Ninawashukuru mmetoa wazo hilo na nitalichukua kwenda kushauriana na wenzangu. Nitatoa maoni na ushauri. Ninadhani kuna jambo linabidi vilevile tulijadili. Tunapenda sana kukabidhi uamuzi wa muundo wa nchi yetu kwenye kikundi kidogo cha wataalamu.

"Ndio maana wakati mwingine unaweza ukawa na mantiki na ukawa na hoja ya kuwa na kijiji au kuwa na mtaa au kuwa na serikali fulani mahali fulani, lakini kwa sababu wanaoamua wako mbinguni, wako kule juu lazima maombi yapelekwe mbinguni kwa wakubwa," alifafanua.

Alisisitiza kuwa hiyo inamfanya afikiri mambo ya msingi yanayohusu maendeleo ya wananchi, lazima yaamuliwe na wananchi na lazima yatokane na wananchi.

"Wabunge wanaona jambo jema, halmashauri kuu ya wilaya inaona jambo jema, madiwani wanaona jambo nzuri, lakini hawana uamuzi nalo," alisema.



Kinana alisema umefika wakati kama kweli madaraka ni ya wananchi, basi wawakilishi wa wananchi wawakilishe wananchi, wawe na kauli katika kuamua juu ya mambo yanayohusu wananchi, nchi isibaki na mfumo na utaratibu wa zamani.

**UTEKELEZAJI ILANI**

Kinana pia alipongeza utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM unaofanywa katika Jimbo la Mtama, akisema kazi nzuri inafanyika kupitia kwa madiwani na viongozi wa halmashauri katika kusimamia utekelezaji wake.

"Ninampongeza Mbunge wenu Nape anatosha. Ni kijana hodari anajituma, nimekaa naye miaka saba, spidi yake ilikuwa kali, kuna wakati nilikuwa ninaipunguza na nilimwambia Nape jifunze kuwa na subira na siku hizi ana subira kuliko mimi," alisema.

Kinana alisema amesomewa taarifa ya chama na taarifa ya serikali, akaangalia kila eneo, likiwamo suala la umeme vijijini, alilosisitiza Mkoa wa Lindi kabla ya kufikia Desemba 2025 vijiji vyote vitakuwa na umeme.

"Mimi nina bahati ya kuzunguka nchini, hivi karibuni nilikuwa Geita na Kagera, na kabla ya hapo nilikuwa Manyara, Tabora na sehemu nyingine. Ninataka niwahakikishie ndugu zangu itakapofika 2025 vijiji vyote nchi hii vitakuwa na umeme," aliahidi.

Kinana pia alisema wakati mwingine amekuwa anasikia watu wana malalamiko ya maji, umeme, afya na mengine lakini akiyasikia hayamtishi, bali yanamtia ari.

"Malalamiko ni matokeo ya kazi nzuri inayofanyika, kila tukipiga hatua watu wanadai hatua mara mbili, si wanalalamika kazi haifanyiki hapana! Wanasema kama mmeweza kufanya kiasi hiki, tunaomba basi mfanye mara mbili, mara tatu, mara nne.

"Maana yake kama mmeweza kupeleka umeme vijiji vyote sasa tunataka mpeleke kwenye vitongoji na mitaa yote, ndio maana yake! Maendeleo yanaleta hamu kubwa zaidi ya maendeleo. Kwahiyo, yanaleta madai makubwa zaidi," alisema Kinana.

Aliongeza kwamba katika mkutano huo wananchi wamemsikia Meneja wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) Mkoa wa Lindi, Irene Kataraihya akizungumza kuhusu bima ya afya, akiwaambia kuwa kuna sheria imepitishwa bungeni.

"Jambo moja hajawaaambia sheria hii imerudi bungeni mara nne, mara ya kwanza ikaboreshwa, mara ya pili ikaboreshwa, mara ya tatu ikaboreshwa na mara ya nne hatimaye ikapita kuwa sheria.

"Lengo lake ni moja kumpa huduma bora kila mtanzania na hata hizi kelele ndogondogo mnazosikia ni kelele la kufanya jambo lenyewe liwe nzuri zaidi.

"Kwahiyo, nikisikia kelele watu wanazungumza changamoto unakaa unatakari, unasema hapa watu wanachotaka jambo hilo liwe nzuri zaidi," alisema.

**ALICHOSEMA NAPE**

Awali akizungumza katika mkutano huo, Mbunge wa Mtama ambaye pia ni Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape, alikiomba chama kutazama upya uamuzi wa kutanua maeneo ya kiutawala hususan kwa ngazi ya vijiji na vitongoji.

Kwa mujibu wa Nape, baadhi ya maeneo kuna hali ngumu kuwahudumia wananchi kutokana na ukubwa wa maeneo na wingi wa wananchi, hivyo ni vyema kuridhia kuyaongezea maeneo ya kiutawala.

Nape alisema kuwa kutokana na wingi huo na umuhimu wa kuwahudumia wananchi, alikiomba chama kiridhie kuanzishwa kwa vijiji na vitongoji vipya kusaidia kuwahudumia wananchi kwa ufanisi.


Kuhusu utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi, Nape alisema serikali imefikisha huduma muhimu katika jimbo hilo.

Miongoni mwa huduma hizo ni maji safi na salama, ujenzi wa vituo vya afya na zahanati, kufungua mawasiliano ya simu za mkononi na kusambaza umeme.

Meneja wa NHIF Lindi, Irene, alikiomba chama kuendelea kuwahamasisha wananchi kujiunga na huduma hizo kujihakikishia matibabu wakati wote.

Ali Likalambile, mkazi wa kijiji cha Londo, wilayani humo, alimpongeza Kinana kwa kuona umuhimu wa wananchi kushirikishwa katika kuamua mambo yanayohusu maendeleo yao.

**KABWELA** FADHILI MOHAMED



MAKALA MAALUM

# Waliogeuza mikopo ya makundi maalum kuwa maficho ya ulaji wachukuliwe hatua

**Na Mwandishi Wetu**

MWAKA 1993, serikali kupitia Bunge, ilianzisha kisheria Mfuko wa Fedha wa Maendeleo kwa Wanawake na Vijana ili kuwainua wanawake na vijana wasiojiweza kiuchumi ambao wengi wao hawakidhi vigezo vya mikopo inayotolewa na taasisi za fedha kutokana na ukosefu wa dhamana.

Kwa wakati huo, mikopo hiyo ya uwezeshaji ilitolewa asilimia tano kwa wanawake na asilimia tano kwa vijana.

Mnamo mwaka 2019, serikali kupitia Bunge, ilirekebisha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290 (iliyorejewa 2019) kwa kuongeza kifungu cha 37A mahususi kuwezesha mikopo kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Kifungu cha 37A(1) cha sheria hiyo kinazitaka halmashauri zote kutenga asilimia 10 ya mapato yao ili kutoa mikopo isiyo na riba kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu vilivyosajiliwa.

Vilevile, Kanuni za Utoaji na Usimamizi wa Mikopo kwa Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu, 2019 (Tangazo la Serikali Na. 286 la 5/04/2019) zinataka mamlaka zote za serikali za mitaa kutenga asilimia 10 ya mapato yatokanayo na vyanzo vya ndani ili kutoa mikopo isiyo na riba kwa vikundi vilivyosajiliwa vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Madhumuni ya mfuko huo ni kuongeza uwezeshaji kiuchumi kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa kufanya shughuli za kiuchumi ili kuboresha kiwango chao cha maisha.

Ili kuwezesha mfuko uwe hai, Mamlaka za Serikali za Mitaa zinapaswa kuhakikisha kuwa fedha zinazokopeshwa kwa vikundi zinarejeshwa kwa mujibu wa makubaliano kati ya mamlaka za serikali za mitaa na vikundi vinavyonufaika na mkopo huo.

Hata hivyo, licha ya kuwa na angalizo hilo la kisheria, mikopo hiyo kwa makundi maalum imegeuzwa kichaka cha ufisadi wa mabilioni ya umma.

Kwanini? Katika miaka sita ya fedha iliyopita, yaani kuanzia mwaka 2016/17 hadi 2021/22, jumla ya Sh. bilioni 192 hazijarejeshwa na wanufaika wa mikopo hiyo huku Rais Samia Suluhu Hassan akikiri fedha hizo hazikusanyiki tena kutokana na vikwazo mbalimbali ikiwamo kukopeshwa kwa 'watu hewa'.

Katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka 2020/21 iliyowasilishwa bungeni Aprili 12, 2022, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), alibaini mabilioni ya shilingi yako hatarini kupotea kutokana na kutokuwa na udhibiti mzuri wa usimamizi wa mikopo inayotolewa na halmashauri kwa makundi maalum.

CAG Charles Kichere alibainisha kuwa kwa mwaka huo wa ukaguzi, halmashauri 155 hazikukusanya Sh. bilioni 47.01 za marejesho ya mikopo iliyotolewa kwa makundi hayo.

Kwa mujibu wa CAG, hali iliyobainika katika ukaguzi wake wa mwaka 2020/21, ni mwendelezo wa kile alichokibaini katika miaka mitano iliyopita kuhusu mikopo hiyo.

| Mwaka | Hal | Kisichorejeshwa | % |
|---|---|---|---|
| 2020/21 | 155 | Bil. 47/- | 70 |
| 2019/20 | 130 | Bil. 27.79/- | 65 |
| 2018/19 | 111 | Bil. 13.79/- | 59 |
| 2017/18 | 90 | Bil. 10.04/- | 59 |
| 2016/17 | 84 | Bil. 5.81/- | 63 |

Mikopo isiyorejeshwa inayotolewa na serikali kwa makundi maalum kupitia asilimia 10 ya mapato ya halmashauri nchini. **CHANZO: RIPOTI YA CAG 2020/21.**

Vilevile, katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2021/22 iliyowasilishwa bungeni Aprili 6, 2023, CAG Kichere anabainisha kuwa Sh. bilioni 88 zilizokopeshwa na halmashauri kwa makundi maalum kwa mwaka huo wa fedha, hazijakusanywa.

Hii ina maana kwamba kuanzia mwaka wa fedha 2016/17 hadi 2021/22, jumla ya Sh. bilioni 192 hazijakusanywa kutoka kwa wanufaika wa mikopo hiyo.

Katika ripoti yake ya 2020/21, CAG Kichere anabainisha kuwa katika kufuatilia uzingatiaji wa matakwa ya sheria iliyopo, alibaini wanufaika wa vikundi katika mamlaka 155 za serikali za mitaa hawakurejesha Sh. bilioni 47.01 kama marejesho ya mkopo waliopewa.

CAG pia anasema alibaini mamlaka 83 za serikali za mitaa hazikuchangia Sh. bilioni 6.68 katika mfuko kama inavyotakiwa kisheria, jambo ambalo linazuia azma ya serikali ya kuwawezesha kiuchumi wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa lengo la kupunguza umaskini.

"Pia nilibaini mikopo yenye thamani ya Sh. milioni 178.61 ilitolewa kwa vikundi visivyokuwa na sifa na Sh. bilioni 1.24 hazikuhamishwa kutoka akaunti za amana za Mamlaka 11 za Serikali za Mitaa (halmashauri) kwenda akaunti maalum ya mfuko, kinyume cha Kanuni ya 22(1) na (2) ya Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu," CAG anabainisha.

Anazitaja halmashauri ambazo hazikuhamishia Sh. bilioni 1.24 katika akaunti maalum za mikopo ni: Ushetu (Sh. 308,528,550); Bahi (Sh. 54,222,488); Iringa (Sh. 236,486,588); Busega (Sh. 49,090,000); Nanyumbu (Sh. 179,268,173); Momba (Sh. 41,795,000); Kilolo (Sh. 122,596,622); Gairo (Sh. 38,679,672); Rungwe (Sh. 115,777,111); Ileje (Sh. 32,043,700); na Sengerema (Sh. 59,511,900).



Rais Samia Suluhu Hassan akipokea taarifa ya ukaguzi kwa Mwaka 2021/2022 kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Charles Kichere Ikulu Dar es Salaam Machi 29,2023 **PICHA:MTANDAO.**

CAG anabainisha kuwa kutorejeshwa kwa mikopo hiyo kunatokana na kutokuwa na udhibiti mzuri wa usimamizi wa mikopo, akifafanua kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa husika zilitoa mikopo kabla ya kufanya uchambuzi wa kina wa historia ya ulipaji wa kikundi na kupitia mapendekezo ya mradi husika ili kuhakikisha kikundi kina uwezo wa kurejesha mkopo kwa wakati.

Vilevile, CAG anasema amebaini hakuna ufuatiliaji wa karibu wa kukusanya marejesho ya mikopo ambayo haijalipwa kutoka kwenye vikundi.

Anasema ni dhahiri kuwa kutorejeshwa mikopo kunaweza kuathiri mfuko, hivyo kuufanya usiwe endelevu.

Ili kufikia lengo na uendelevu wa mfuko, CAG anasisitiza Mamlaka za Serikali za Mitaa kufanya tathmini kabla ya kutoa mikopo na kuweka juhudi zaidi katika kukusanya madeni ambayo hayajalipwa.

Pia anaishauri Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ianzishe hatua madhubuti za kurejesha mikopo kwa kuhusisha wataalamu wa usimamizi wa mikopo ambao watahimiza uzingatiaji wa urejeshaji wa mikopo kwa hiari ili kufikia ukuaji endelevu wa mfuko.

CAG pia anabainisha kuwa tathmini aliyoifanya katika akaunti za benki za biashara ambako Mamlaka za Serikali za Mitaa hutunza fedha za mfuko, ilibainisha Sh. milioni 156.23 za mfuko zililimbikizwa katika akaunti kwa zaidi ya mwaka mmoja bila kukopeshwa kwa wanufaika pasi na sababu za msingi.

Halmashauri zilizokuwa na bakaa ya muda mrefu katika benki za biashara ni za wilaya za Mpwapwa (Sh. 108,703,450) na Nyasa (Sh. 47,530,700).

CAG anataja dosari nyingine katika mikopo hiyo ni kutoshirikishwa wataalamu wa usimamizi wa mikopo katika mchakato wa utoaji na urejeshwaji mikopo.

Anafafanua kuwa Kanuni ya 8 ya Kanuni za Utoaji na Usimamizi wa Mikopo ya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu za Mwaka 2019, inataka taratibu zote za wa mikopo zisimamiwe na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

"Tathmini niliyoifanya ya taratibu zinazopaswa kuzingatiwa wakati wa utoaji wa mikopo kwa vikundi vilivyosajiliwa, ilibaini changamoto kadhaa ikiwa ni pamoja na uwezo duni wa Idara za Maendeleo ya Jamii katika ngazi ya halmashauri katika kutoa, kufuatilia na kusimamia urejeshwaji mikopo hiyo na kutoa huduma za maendeleo ya kibiashara kwa wanufaika, jambo ambalo linapunguza uwezo wa mfuko kufanya kazi ipasavyo.

"Pia nilibaini kuwa uhakiki wa vikundi vilivyoomba mikopo ulikuwa haufanyiki kabisa kabla ya mikopo kutolewa. Hii ni kutokana na ukosefu wa utaalamu wa kufanya uhakiki unaostahili katika mikopo.

"Pia kukosekana usaidizi wa kisheria kutoka katika vitengo vya sheria kuhusu masuala ya bima hasa kwa mikopo inayotolewa kwa vijana, ambao mara nyingi walikuwa wakinunua pikipiki na bajaji. Mfuko hauna sera ya jinsi ya kushughulikia mikopo isiyolipika (NPL)," CAG Kichere anasema.

Anabainisha kuwa kati ya madeni hayo, yapo ambayo yameonekana dhahiri hayatolipika kutokana na kuwa chechefu au madeni hewa na hivyo kuendelea kuudhoofisha mfuko.

Baada ya kupokea ripoti ya CAG kwa mwaka 2021/22 ikionesha kwa mwaka huo wa ukaguzi, Sh. bilioni 88 zilizotolewa na halmashauri kama mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na wenye ulemavu hazikurejeshwa, Rais Samia Suluhu Hassan alisema kadhia hiyo inasababishwa na utaratibu mbovu wa utoaji mikopo hiyo na ufuatiliaji hafifu.

"Sh. bilioni 88 zimekwenda, hazijakusanywa na hazikusanyiki, na hii ni kwa sababu vikundi vinavyopewa ni hewa, uadilifu kwa madiwani ni hewa na pili wanaopewa wanaona wamepewa na madiwani wao, hawaoni umuhimu wa kurejesha. Kwahiyo, tunahitaji marekebisho makubwa," alisema Rais Samia.

Marekebisho yanayotajwa na Rais Samia yanahusu kubadili mfumo wa utoaji mikopo hiyo kutoka halmashauri ili kazi hiyo ifanywe na benki ambayo itakuwa imeteuliwa na serikali kusimamia jambo hilo, ushauri ambao ulitolewa na CAG katika ripoti ya mwaka 2020/21.

"Njia itayotufaa ni ya kutumia mfumo wa benki, tupige hesabu ya asilimia 10 inayohitajika katika halmashauri husika kisha ikakae benki, wanaohitaji mikopo watakwenda benki, kwa sababu benki uwe unataka au hutaki, lazima utarejesha," alisema Rais Samia.

Mwishoni mwa mwaka uliopita, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, aliagiza wizara husika kurejesha mikopo hiyo serikali kusitisha kuitoa, lakini hatua dhidi ya waliosababisha ufujaji wa mabilioni hayo hazijachukuliwa.

Ufujaji wa fedha hizo si tu unakwaza kufikiwa malengo ya uanzishwaji wa mfuko wa kuinua wanawake na vijana wasiojiweza kiuchumi, bali pia unakwaza utekelezaji Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025, yenye lengo kuu la kupunguza walau nusu ya wananchi wanaoishi katika umaskini na kuwafanya waishi katika uchumi wa kati ifikapo mwakani.

# Samia awapa vyakula watoto wa wafungwa

**Na Allan Isack,** ARUSHA

RAIS Dk.Samia Suluhu Hassan ametoa zawadi ya vyakula vyenye thamani ya Sh.milioni 4.3 kwa watoto wanaoishi kwenye makao ya kulelea watoto mkoani hapa kwa ajili ya kusheherekea sikukuu ya mwaka huu mpya wa 2024.

Zawadi hizo zilizotolewa jana kwa Makao ya St. Gabriel ya jijini Arusha yanayowalea watoto ambao wazazi wao wanatumikia vifungo katika magereza mbalimbali nchini na Makao ya Dhi Nureyn yaliyopo Ngaramtoni Wilaya ya Arumeru ni pamoja na mchele, sukari, unga wa ngano na sembe, maharage, mafuta ya kula, juisi na biskuti.

Akikabidhi zawadi hizo Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongella alisema kuwa ametoa zawadi hizo kwa niaba ya Rais Samia ikiwa ni ishara ya upendo, amani na moyo wake wa kipekee wa kuwajali watoto wenye mahitaji na waishio kwenye makao hayo ili na wao wajisikie kama walivyo watoto wengine wa Kitanzania.

"Mheshimiwa Rais amenituma kuleta zawadi hizi kwa niaba yake kwa kuwa ni kawaida yake ikifika msimu wa sikukuu hupenda kutoa zawadi kwa watoto wanaolelewa kwenye makazi yanayolea watoto wenye uhitaji nchini," alisema Mongella.

Amewapongeza walezi wa watoto hao kwa kazi kubwa wanyoifanya kwa kuwa jukumu hilo lina thamani na thawabu kubwa kwa binadamu na zaidi kwa Mwenyenzi Mungu.

"Zawadi hii pia inaonyesha namna Serikali inavyothamini kazi kubwa inayofanywa na walezi kwa kuwa wanaisaidia katika suala la malezi ya watoto, hususani hawa wenye mahitaji maalumu kutokana na changamoto nyingi zilizowafikisha hapo," alisema Mongela.

Akizungumza baada ya kupokea zawadi hizo, Kiongozi wa Makao hayo, Mtawa Marieta Muyegi amemshukuru Rais Samia na Serikali yake kupitia Mkuu wa Mkoa wa Arusha kwa kuonyesha upendo wa hali ya juu kwa watoto wanaowalea.

"Tufikishie salamu zetu kwa Rais Samia, tunatambua mchango wa Serikali kwa kuweka mazingira wezeshi ya kuwalea watoto wenye uhitaji nchini, vituo hivi vinafanya kazi kutokana na sera nzuri za Serikali," alisema Mariethа.

Akizungumza kwa niaba ya watoto wenzake, Florentina Mbisha wamemshukuru Rais Samia kwa zawadi hizo na kumuombea kwa Mwenyenzi Mungu amzidishie pale alipotoa na kumpa baraka nyingi katika maisha yake na uongozi wake..



Baadhi ya watoto wa mjini Babati, mkoani Manyara, wakisherehekea Sikukuu ya mwaka mpya wa 2024 kwa kuogelea kwenye kituo cha Negamsi Park, jana. **PICHA: GIFT THADEY**

## CCM kuwatosa viongozi hawa uchaguzi wa mitaa

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Tanga, Rajabu Abdallah amesema chama hicho hakitawanadi viongozi wachafu na wasiouzika kwa wananchi katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa utakaofanyika nchini mwaka huu.

Akizingumza juzi katika Kata ya Kange ya Halmashauri ya Jiji la Tanga, Abdallah alisisitiza kuwa kwa Mkoa wa Tanga hakuna shida kwani kuna mshikamano baina ya viongozi wa chama na wa Serikali.

Licha ya kusisitiza ushirikiano na mshikamano kwa lengo la kuunga mkono juhudi za Rais Dk. Samia Suluhu Hassan katika utendaji kazi wake, alisema kwenye uchaguzi huo CCM hakitawabeba viongozi na wanachama wake wasioweza kubebeka.

Alisema katika uchaguzi huo, CCM kimejidhatiti kushinda kwenye nafasi zote kuanzia ngazi ya vitongoji, vijiii na mitaa lengo ni kuufanya Tanga kuwa na utawala wa chama kimoja bila upinzani.

"Zimebaki siku chache tunaingia uchaguzi Serikali za Mitaa, hatutapoteza kiiiji, mtaa wala kitongoji, naomba niwahakikishie kwamba mnaye nahodha mzuri ndani ya CCM," alitamba Abdalla.

Pamoja na mambo mengine, alisema kuanzia uchaguzi huo wa mitaa kuelekea uchaguzi mkuu, ni lazima CCM kiwekw watu watakaouzika ili kukiwezesha kupata nafasi ya kuwanadi vizuri.

"Chama Mkoa hatutafanya kazi ya kuwanadi watu wachafu, waliokaa kwenye uongozi miaka mitano hata mikutano kwa wananchi hakuna, tutafanya utafiti wa kutosha nani anauzika," alisema na kuongeza:

"2025 ni uchaguzi rais, wabunge na madiwani, tutashinda maeneo yote, tuendelee kushikamana kama kuna mtu anakosea aelezwe kwa busara. Kanuni, taratibu na sheria kuzingatiwa bila mtu kusubiri chama kumshughulikia."

**Pamoja na mambo mengine, alisema kuanzia uchaguzi huo wa mitaa kuelekea uchaguzi mkuu, ni lazima CCM kiwekw watu watakaouzika ili kukiwezesha kupata nafasi ya kuwanadi vizuri.**

# Mgogoro sugu wa hifadhi, wanakijiji wabaki historia

**Na Allan Isack,** KARATU

MGOGORO wa mpaka kati ya Kijiji cha Buger kilichopo wilayani hapa na Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara uliodumu zaidi ya miaka 15 iliyopita sasa umebaki historia baada ya kupatiwa ufumbuzi na Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongella.

Mongella juzi alitangaza kwisha kwa mgogoro huo baada ya kamati ndogo aliyounda kujumuisha wataalamu na wawakilishi wa wananchi hao kupata suluhisho la kudumu kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika kijijini hapo.

Alisema kamati hiyo imetoa uamuzi ambao umegusa pande zote kwa kila mmoja kuathirika kwa kumegwa eneo lake.

Alisema eneo la hifadhi lenye ukubwa wa hekari 8.3 limemegwa na kuachiwa wananchi na eneo lililojengwa nyumba tatu za wananchi likiachiwa ili waendelee kumiliki.

Mongella aliwataka wananchi hao kuachana na mgogoro na kujikita kufanya kazi za uzalishaji mali na miradi ya maendeleo kwa manufaa ya familia zao na taifa. "Kila mwananchi ana wajibu wa kulinda eneo la hifadhi kwa kutambua thamani yake, ambayo wananchi wa Buger wananufaika nayo, mnapata unyevuunyevu ambao unawawezesha kufanya kilimo cha mwaka mzima, hii ni kutokana na uwepo wa eneo la hifadhi linalotunzwa, hivyo ni wajibu wetu kuendelea kutunza eneo hili kwa manufaa yetu na vizazi vijavyo," alisisitiza.

Vilevile aliuagiza uongozi wa hifadhi hiyo kuanza kuweka alama kwa kuzingatia vipimo vya mipaka iliyokubalika na kuweka barabara ili wananchi watambue mipaka yao.

Akisoma uamuzi ya kamati hiyo, Mkuu wa Hifadhi hiyo, Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi, Eva Mallya, alisema mpaka huo umezingatia maslahi ya pande hizo.

Eva alisema takribani hekari 8.3 za hifadhi, nyumba tatu za wananchi na kisima cha maji zilizojengwa eneo la hifadhi limeachiwa wananchi huku baadhi ya vipande vya ardhi ambavyo walikuwa wakilima vikirudiishwa kwenye hifadhi.

Ofisa Ardhi Mkoa wa Arusha, Daniel Mruma alisema kuwa Idara ya Ardhi imeshirikiana na timu iliyoundwa na Mongella na pande hizo kufikia mwafaka wa hifadhi kuachia hekari 8.3 na kazi inayofuata ni kuweka alama mpya za mipaka kwenye maeneo hayo.

Hivi karibuni Mongella alikutana na wananchi hao na kujadili mgogoro huo na kuunda kamati ya makubaliano ambayo imekuja na suluhisho la kudumu la mgogoro huo.





# Madereva kunyang'anywa leseni kwa kuchezea VTS

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

KIKOSI cha Usalama Barabarani kimeonya kuwa kitawanyang'anya leseni madereva wa mabasi ya abiria watakaobainika kuchezea Mfumo wa Udhibiti Mwendo (VTS) kwa lengo la kuendesha kwa mwendo kasi na kuhatarisha maisha ya abiria.

Onyo hilo lilitolewa juzi na Mkuu wa Dawati la Elimu wa kikosi hicho, Michael Deleli wakati akitoa elimu ya usalama barabarani katika Kituo Kikuu cha Mabasi Kahama mkoani Shinyanga.

Deleli alisema ajali nyingi zinazotokea barabarani nchini, zinasababishwa na madereva wasiokuwa waadilifu wawapo safarini kwa kuchezea VTS kwa lengo la kuwahi kufika safari zao kwa kuendesha mabasi kwa mwendo kasi bila kujali kuwa wanahatarisha maisha ya abiria.

Alisisitiza kuwa watakaobainika kuchezea VTS, watachukuliwa hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kunyang'anywa leseni zao kwa kukiuka sheria kwa sababu kifaa hicho kimewekwa kwa lengo la kudhiti mwendo dereva anapojisahau awapo safarini.

Aliwataka madereva wa mabasi wanaofanya safari ndefu zaidi ya saa nane kuhakikisha wanakuwa na dereva wa akiba wa kuwapokea ili kuepuka ajali kutokana na uchovu na usingizi.

Mmoja wa abiria aliyekuwa akisafiri kuelekea mkoani Kigoma, Lameck Samweli, alisema madereva wana nafasi kubwa ya kudhibiti ajali kutokea kwa kuzingatia sheria na alama za barabarani.

Dereva wa basi la Adverture linalofanya safari Kahama hadi Kigoma, Issa Hamisi alisema kuna baadhi yao wanachezea mfumo huo ili kuendesha mabasi kwa mwendo kasi na kuwahi kufika wanakokwenda.

Hamisi alikiomba kikosi hicho kuwachukulia hatua madereva hao ili iwe fundisho kwa wengine wenye tabia hiyo kwani wanahatarisha maisha ya abiria wanaosafiri kwenye mabasi yao..



Uongozi wa chama Kikuu cha Ushirika Kahama (KACU), wakifurahia kwa pamoja na watoto wanaolelewa na kituo cha New Hope Center kilichopo Mtaa wa Mwine ilindi, kata ya Zongomela Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, kama sehemu ya kuukaribisha mwaka mpya wa 2024, kwa kuwapatia mahitaji mbalimbali yenye thamani ya Sh. milioni moja jana. **PICHA: SHABAN NJIA.**

## KACU yawapatia msaada yatima

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

CHAMA Kikuu cha Ushirika Kahama (KACU) mkoani Shinyanga kimewapatia zawadi watoto wa kituo cha kulelea yatima cha New Hope Center kilichopo Mtaa wa Mwime Ilindi Kata ya Zongemala Halmashauri ya Manispaa ya Kahama kwa ajili ya kusheherekea mwaka mpya 2024.

Mwenyekiti wa chama hicho, Tano Nsabi akikabidhi zawadi hizo jana, alisema wamekuwa na utaratibu wa kutembelea vituo vya kulelea watoto yatima kila mwaka na kuvipatia mahitaji muhimu kama sehemu ya kurejesha faida wanayopata kwenye uuzaji wa zao la pamba, tumbaku na mengine mchanganyiko.

Nsabi alitaja vitu vilivyotolewa kituoni hapo kuwa ni pamoja na mchele, maharage, unga, mafuta ya kula, sabuni, madaftari, soda na sukari vyenye thamani ya Shilingi milioni moja, na kuyataka makundi mengine kujenga tabia ya kutembelea vituo hivyo na kutoa mahitaji.

Aliwataka viongozi wa kituo hicho kuhakikisha watoto hususani wanafunzi wanatimiza ndoto zao ili kukisaidia kituo hicho baadaye.

Mkurugenzi wa kituo hicho, Seleman Juma, alishukuru uongozi wa chama hicho kwa kuwakumbuka na kuwapatia zawadi hizo kwani wamekuwa na uhitaji mkubwa hasa kwa wanafunzi.

Alisema maisha ya watoto hao yanategemea misaada ya wahisani na kuwahakikishia inatumika kwa malengo ya kuwalea bila ubaguzi.

Akizungumza kwa niaba ya watoto hao, Salome Godfrey alishukuru kwa msaada huo na kuwaomba vifaa vya shule hasa madaftari na sare.

# Wananchi wamkuna RC kudumisha amani

**Na Vitus Audax,** MARA

WAKAZI mkoani hapa, wametakiwa kuendelea kulinda amani na kujiepusha na matukio ya uvunjifu wa amani katika kipindi cha mwaka huu wa 2024.

Rai hiyo ilitolewa na Mkuu wa Mkoa wa Mara, Said Mtanda juzi ofisini kwake wakati akizungumzia jinsi walivyofanikiwa kudhibiti vitendo vya uhalifu mkoani hapa katika kipindi cha mwaka jana.

Mtanda alisema hakuna vitendo vyovyote vya uhalifu wala ukatili vilivyotokea kama ilivyokuwa ikiripotiwa na kuwataka wakazi hao kuendelea kulinda na kudumisha amani kwa kipindi cha mwaka huu.

Alisema wakati anakabidhiwa mkoa huo, alikuta tukio la vifo vya waendesha bodaboda watano waliouawa kwa kuchinjwa wilayani Butiama na alihakikisha wauaji wamekamatwa na kufikishwa katika vyombo vya sheria.

"Niwahakikishie kuwa mkoa upo salama hauna tishio lolote na baada ya tukio hilo kubwa tulifanya operesheni ndani ya wiki moja na kila muhusika alikamatwa na sheria inaendelea kuchukua mkondo wake dhidi yao," alisisitiza

Akizungumzia kuhusu Sikukuu za Krismasi na Mwaka Mpya 2024 mkoani hapa, alisema zimesherehekewa kwa utulivu baada ya Serikali kufanikiwa kudhibiti vitendo vya uhalifu ikilinganishwa na vilivyojitokeza kipindi kizima cha mwaka jana.

" Ni jukumu la wananchi kuendelea kuilinda hii tunu yetu muhimu ya amani na utulivu vilivyodumu kwa muda mrefu nchini," alisema Mtanda.

Akizungumzia kuhusu mwaka huu mpya wa 2024, alisema mkoa huo unatarajia kuendelea kutatua migogoro ya ardhi ili kuhakikisha inakwisha.

Mwaka jana Mara ulikumbwa na matukio mbalimbali ikiwemo mgogoro wa mpaka wa Nyanungu na Hifadhi ya Serengeti.

Aliyekuwa Mkuu wa Mkoa huo, Meja Jenerali Suleiman Mzee alipiga marufuku wakazi wa Kata ya Nyanungu Wilaya ya Tarime kujishughulisha na kilimo katika eneo la mlima linalopakana na Hifadhi ya Taifa ya Serengeti (SENAPA).

Katika mgogoro huo, wananchi walidaiwa kumuua askari wa SENAPA kwa kumchoma kwa mshale wenye sumu wakati akitekeleza majukumu yake katika eneo hilo kitendo kilichokemewa vikali na mkuu huyo wa mkoa.

Amri ya kuwazuia wananchi kufanya shughuli za kibinadamu katika eneo hilo iliibua Mbunge wa Tarime Vijijini, Mwita Waitara kwa kuwataka kumuunga mkono katika mapambano ya kuwapigania huku akionekana kuangua kilio katika vyombo vya habari na kutoka nje ya Bunge kwa kile alichodai kuwa hoja yake haikusikilizwa.

Usiku wa kuamkia Mei 28, mwaka jana watu wanne,wakiwemo waendesha bodaboda watatu waliuawa kikatili kwa kushambuliwa na kuchomwa miili yao na pikipiki zao kutelekezwa katika vichaka nje kidogo na Kijiji cha Nyakiswa Kata ya Kyanyari wilayani Butiama.

Kamishna wa Oparesheni na Mafunzo ya Jeshi la Polisi, Awadhi Juma aliongoza msako maalumu na kuwakamata watuhumiwa hao ndani ya wiki moja na kufikishwa mahakamani kujibu mashtaka ya mauaji.

Nipashe
# TESA
Jumanne Januari 2 , 2024
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI




Ukurasa 13



Ukurasa 12

Miaka 50 Chuo cha Ustawi wa Jamii, inaposherehekewa kwa jukumu jipya



Ukurasa 14

'Hata ukikimbia kidogo una faida milioni kiafya'

ELIMU

NA GRACE MWAKALINGA, PWANI

# Shule shikizi inabaki kuwa nguzo inayomfungua mtoto

## •Inamuinua na kumuanzisha kiakili, kukuza uelewa

HERI ya mwaka mpya 2024. Pazia la mwaka linapofunguka, Januari 8 wiki ijayo, shule zinafunguliwa mzazi mwanao anaanzia wapi? Darasa la shikizi au la kwanza ama ngazi ya juu zaidi, ulimwandaa kikamilifu kwa kumsomesha elimu ya awali? Kama hukufanya hayo fahamu 'ulichemka' kwa sababu hatua hiyo ni muhimu kama wataalamu wanavyofahamisha.

Elimu ya awali inayopewa majina mengi kama chekechea, kindegateni na sasa shikizi ni muhimu, tena kuna tofauti kubwa kati ya aliyepata elimu ya awali na mtoto ambaye hakusoma chekechea kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Chuo cha Cambridge cha Uingereza.

Unabainisha kuwa jinsi mtoto anavyokuwa darasani kiwango chake cha akili na uelewa wa mambo kinakuwa kikubwa kuliko aliye mtaani, akisubiri aingie darasa la kwanza moja kwa moja.

Watafiti hao wanasema elimu hiyo humwezesha mtoto kushiriki shughuli za elimu ya awali zinazomwezesha kuwa na msingi bora wa maarifa, stadi, na tabia zinazomwezesha kuanza shule ya msingi.

Darasa la awali ni muhimu kwa mtoto, elimu anayoipata inamsaidia kuongeza kasi ya ubongo wake kuhifadhi, kuchambua, kugundua na kufanya maamuzi sahihi hata atakapokuwa mtu mzima, wanaongeza watafiti hao, pia wanataja kumsaidia ajitambue na kuyapenda mazingira ya shule.



Mwalimu wa shule ya awali akiwafundisha watoto wenye umri wa shule shikizi kupitia mradi wa LEARN Plus unaofanikishwa na Plan International wilayani Kisarawe. **PICHA:GRACE MWAKALINGA.**

Mwaka 2015, Tanzania iliridhia Malengo 17 ya Maendeleo Endelevu (SDGs) yaliyowekwa na Umoja wa Mataifa (UN) kufikiwa ifikapo mwaka 2030 ili kushughulikia masuala mbalimbali kwa ustawi wa raia wake.

Lengo namba nne linasisitiza elimu bora, sawa na endelevu pamoja na kuendeleza fursa za kujifunza kwa raia wote, hilo linaweza kufanikiwa iwapo zipo sheria na sera ambazo zinawezesha elimu kumfikia kila mmoja.

Shirika la Plan International ni moja ya wadau wanaoshirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, TAMISEMI na ile ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu kwenye mradi wa LEARN Plus, uliozinduliwa Januari 2021, ukitekelezwa kwa miaka mitatu, anasema mratibu wa mradi, Creptone Madunda.

LEARN Plus, inalenga kuwaandaa na kuwawezesha watoto wenye umri wa miaka mitano hadi sita kuanza darasa la kwanza kufuatia utafiti uliofanyika katika Wilaya ya Kisarawe mkoani Pwani kubaini sababu zinazochangia watoto wa umri wa shule ya awali kushindwa kuanza kusoma.

Utafiti huo ukifanywa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Kituo cha Utafiti cha Maendeleo Kimataifa (IDRC), ukiwalenga watoto wenye umri wa miaka mitano na hadi sita waliokosa elimu ya awali na wakikaribia kujiunga na darasa la kwanza kutokana na kigezo cha umri , ulibaini changamoto kadhaa ikiwamo umbali mrefu kwenda shule, kukosa usalama, wanyama wakali, mila na desturi zinazokwamisha elimu ya awali.

Tafiti zilifanywa katika kata 12 wilayani Kisarawe zikilenga kuibua changamoto zilizopo na mapendekezo ya kuboresha mazingira ya kutoa elimu ya awali na msingi nchini.

Mradi wa LEARN Plus ulianza mwaka 2021 na unatarajiwa kumalizika 2024, ukitekeleza shughuli mbalimbali kama kufanya uhamasishaji wa jamii kuhusu umuhimu wa elimu ya awali, kuanzisha madarasa ya vituo vya utayari, kutengeneza dhana za kuchezea na kujifunzia, kugawa vifaa vya kupikia chakula cha watoto, kutoa mafunzo kwa walimu wasaidizi wa jamii pamoja na walimu wa darasa la kwanza.

Kadhalika kutoa mafunzo ya kupanga, kutekeleza, kusimamia na kuangalia ubora wa utekelezaji wa mradi, kufunza elimu ya malezi kwa wazazi na walezi wa waoto vituoni, kufanya utafiti wa utekelezaji wa mradi pamoja na utafiti wa tathimini ya matokeo ya mradi, anasema Creptone Madunda.

Mratibu wa mradi wa LEARN Plus, Creptone Madunda, anasema mradi unalenga kusaidia kufikia lengo la namba 4.2 linalosisitiza kutoa elimu bora, sawa, na endelevu pamoja na kuendeleza fursa za kujifunza kwa wote bila kujali asili, jinsi au hali.

Anasema katika kufanikisha mradi huo kwa kushirikiana na serikali walitoa mafunzo kwa walimu waliochaguliwa katika maeneo yao ili kuwafundisha na kuwaandaa watoto kwenye vituo 29 ambavyo vilianzishwa kutoa elimu ya awali, wakifundishwa mbinu na stadi mbalimbali za ufundishaji na namna ya kuwahudumia watoto ili wapate elimu na maarifa yatakayowasaidia kipindi watakapojiunga na darasa la kwanza.

Masha Mohhamed ni miongoni mwa walimu wa elimu jamii (WWJ), aliyejengewa uwezo kufundisha watoto katika kituo cha Chole wilayani Kisarawe, anayefundisha watoto 20 na kati yao 13 tayari wamejua kusoma na kuandika na saba, wenye ulemavu hawajui kutokana ukosefu wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia.

"Ni mwalimu pekee kwenye hiki kituo , nafundisha watoto, vikwazo ni kukosa fedha ya kujikimu, silipwi mshahara ni kazi ya kujitolea lakini kwa sababu nawapenda nalazimika, vitendea kazi vya kufundishia na kujifunzia havitoshi mfano rangi, karatasi na watoto wenye mahitaji maalum kutokuwa na vifaa vyao, anasema Mohhamed.

Anapongeza juhudi akisema kuna mwitikio mkubwa kwa sababu wazazi na walezi wengi wamefurahia watoto wao kujua kusoma na kuandika na kushawishika kuwaandikisha watoto, aidha, elimu hiyo inapatikana jirani hivyo usalama wa watoto ni mkubwa kuliko ilivyokuwa awali kwani walitembea zaidi ya kilomita 10 kwenda pekee.

Ofisa Elimu Watu Wazima, Wilaya ya Kisarawe, Esther Senkoro, pia

INAENDELEA UK.12

ELIMU
NA SABATO KASIKA

# Miaka 50 Chuo cha Ustawi wa Jamii, inaposherehekewa kwa jukumu jipya

JARIDA la TESA linawapa hongera na salamu motomoto wasomaji na watangazaji wetu kwa kufikia mwaka mpya wa 2024, tunawaomba muendelee kutumaini na kuwa nasi katika jukumu la kuwahabarisha, kuwaelimisha na kuwaburudisha.

Wakati mwaka 2023 unapotoweka na sasa ni zama za 2024 taifa linapotazama nyuma linayaona masuala ya ukatili kwa wanawake, watoto, wazee na wahitaji yakivuka mwaka na kuendelea kuwatesa Watanzania bila kujali wapi walipo.

Kwa mfano yapo matatizo mbalimbali ndani ya jamii kama kukithiri rushwa, wizi wa mali ya umma, kuvunjika ndoa, kutelekeza familia, malezi duni ya watoto, ukatili wa kijinsia, ubakaji, ulawiti mauaji ya wanandoa, ushoga na kuunda vikundi vya kihalifu vya vijana wanaoua na kuiba kikiwamo cha 'panya rodi.'

Serikali inaona ni wakati wa kupata majibu ya maswali yanayolenga kuujua ukweli ni nini hasa chanzo cha hali kama hizo? Anayasema hayo Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kwamba taifa linatamani kufahamu chanzo, akikiagiza Chuo cha Ustawi wa Jamii kujikiti kwenye utafiti kufanikisha kufahamu mwanzo ili kumaliza changamoto kama hizo zinazoumiza jamii.

Ni wakati wa maadhimisho ya jubilii ya miaka 50 ya Chuo cha Ustawi wa Jamii jijini Dar es Salaam, yanayofanyika mwezi uliopita, sambamba na Wiki ya Ustawi wa Jamii hapo Desemba 18.

Waziri Mkuu akiwa mgeni rasmi, anaitaka taasisi hiyo kubadili mitaala na kujikita zaidi katika utafiti wa changamoto na matatizo hayo ndani ya jamii, akisema kupitiwa mitaala hiyo ili kujikita katika utafiti, kutasaidia kuja na majibu yatakayosaidia kumaliza 'mbigiri' hizo ndani ya jamii, ambazo zimezuia mazao bora kustawi, hasa kuhusiana na masuala ya malezi na maadili.




Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akizungumza katika maadhimisho ya Jubilii ya miaka 50 ya Chuo cha Ustawi wa Jamii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

Anavitaka vyuo vya ustawi wa jamii kupitia mitaala na kujikita katika utafiti, kwani itakuwa rahisi kuendana na wakati na kupata majibu ya changamoto zinasababisha matukio yanayokwenda kinyume na maadili.

"Serikali ya awamu ya sita itaendelea kutekeleza azma yake ya kuimarisha ustawi wa wananchi kwa kuendelea kufanya maboresho ya mifumo, ufuatiliaji na usimamizi wa masuala ya ustawi wa jamii na kuendelea kutenga fedha za utekelezaji wa afua mbalimbali," anasema.

**MAFANIKIO**

Wakati wa maadhimisho ya miaka 50, Mkuu wa Chuo, Dk. Joyce Nyoni, anaelezea mafanikio ya chuo kwenye jamii nchini na jumuiya ya kimataifa kwamba ni makubwa na ya kujivunia kama kupiga hatua katika kuelimisha na kufanya kazi kwa karibu na wananchi.

"Ninatamani kuona kunakuwa na sheria itakayoratibu huduma za ustawi wa jamii na kuwezesha wanafunzi wetu kuanzisha huduma binafsi," anasema Dk. Joyce akiongeza kuwa ndani ya miaka 50 chuo kimetambulika nje na ndani ya Tanzania, kwa kuwa wamejiunga na shirikisho la vyuo vinavyotoa fani ya ustawi wa jamii Afrika na la dunia.

"Kwetu ni fursa kwani tumeshirikiana na vyuo vingine katika utafiti na kusomesha walimu wetu katika ngazi ya uzamili na uzamivu, wanafunzi wetu kusomeshwa na kwenda nchi nyingine kufanya mafunzo kwa vitendo hivyo kuona namna huduma hizi zinavyotolewa huko," anasema.

Aidha, Dk. Joyce, anasema chuo kilianza kikiwa na wanafunzi takribani 100 wakati huo kikiwa Kurasini Dar es Salaam na sasa kina zaidi ya wanafunzi 5,000 na kampasi moja iliyopo Kisangara wilayani Mwanga mkoa wa Kilimanjaro.

"Chuo pia kilichotoa takriban wanafunzi 18,000 kwenye ustawi wa jamii, rasilimali watu, masomo ya biashara, na ninaona wahitimu wanaweza kushika nafasi ndani na nje ya nchi, kwani mitaala yake inashindana na ya kimataifa hivyo kukubalika kwa masomo na kazi katika vyuo na taasisi za nje."

Mkuu huyo wa chuo anasema, kimekuwa pia kikitoa mafunzo kwa mamalishe na vijana wanaojihusisha na biashara ya chakula, kuimarisha afya ya akili kwa watu mbalimbali.

"Tumetoa huduma hii kwa taasisi na mashirika ya serikali na binafsi, kwani kuna uhitaji na umuhimu wa kutoa elimu kwa jamii ili kuendelea kusaidia jamii ya Kitanzania kuondokana na changamoto mbalimbali," anasema.

Aidha, anasema wanaandaa programu ya saikolojia kwa kuwa kutokana na mabadiliko yanayoendelea, watu wanakutana na changamoto nyingi, na kwamba kuna uhitaji wataalamu wa fani hiyo.

"Tumeshaanzisha programu ya ushirikishwaji wa jamii kwa kuchangamana nayo ili kujifunza na kushiriki kufanya kazi katika jamii, tayari wana programu ya uanagenzi waliohitimu wanaunganisha ile nadharia ya darasani na uhalisia kwenye jamii ili kutatua changamoto za jamii," anasema.

Anatoa mfano kuwa mwaka jana walipeleka wanafunzi 12 Msomera Handeni Tanga wakafanya kazi kama maofisa ustawi kwenye jamii ili wananchi waliohamishiwa eneo hilo kutoka hifadhi ya Ngorongoro mkoani Arusha wanapata huduma zote.

"Hapa walikuwa wanaona kwa uhalisia kile walichojifunza darasani, nasi tunajitahidi kuwekeza katika kuwapa nafasi ya kufanya kazi na jamii, kwani sisi sio kinachojikita kwenye taaluma ya darasani tu," anasema.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, anamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kutoa kibali cha ajira 350 za maofisa wa ustawi wa jamii.

Waziri anasema, Rais ameahidi kuongeza nafasi hizo za ajira kwa maofisa wa ustawi wa jamii, ili kupanua wigo wa upatikanaji wa huduma za ustawi wa jamii, katika mwaka wa fedha wa 2023/2024.

"Lengo la wizara ni kutaka kuona kila palipo na shughuli ya kijamii, anakuwapo ofisa wa ustawi wa jamii, na kwamba hatua hiyo itasaidia huduma za ustawi wa jamii kueleweka na kupunguza vitendo vya ukatili ndani ya jamii," anasema Dk. Dorothy.

Aidha, anasema, kwa sasa uelewa wa wananchi kuhusu huduma za ustawi wa jamii, na kwamba wakati wa Wiki ya Ustawi wa Jamii, watu 7,766 walipatiwa huduma mbalimbali ikiwamo msaada wa kisaikolojia, afya ya akili na utatuzi wa migogoro ya ndoa.

Mbali na huduma hizo, anasema katika maadhimisho hayo yaliambatana na usajili wa kulea watoto kuasili watoto na malezi ya kambo, uchunguzi wa ugonjwa wa macho, huduma kwa kwa walemavu, vyeti vya kuzaliwa.

"Maadhimisho yanalenga kutangaza huduma za ustawi wa jamii na kuzifikisha kwa umma, kwani kwa miaka 50, chuo kimefanya mambo makubwa ikiwamo kuzalisha maofisa ustawi wa jamii wengi ambao wanafanya kazi katika maeneo mbalimbali," anasema.

# Shule shikizi inabaki kuwa nguzo inayomfungua mtoto

**INATOKA UK.11**

mratibu wa mradi huo wilayani humo, anasema LEARN Plus umekuwa na tija kwa jamii kwa sababu umemaliza tatizo la wanafunzi kushindwa kujua kusoma, kuandika na kuhesabu.

Anatolea mfano wa ujenzi wa kituo cha Cholesamvula pamoja na Shule ya Vibula ambazo ni matokeo ya mradi wa LEARN Plus, umefanikisha kumaliza tatizo hilo, kwa kujasili watoto wengi na kutoa fursa wengi zaidi kuandaliwa kujiunga na darasa la kwanza.

Mafanikio mengine ya mradi huo ni kutambulika kwa uhitaji wa kujenga shule kwa baadhi ya maeneo mfano Vibula shule kamili imejengwa, Chole kujengwa darasa moja, Malangalanga madarasa mawili na matundu sita ya vyoo na vituo vingine wamekwisha andaa ardhi na mahitaji mengine kwa ajili ya kuanza au kuendeleza ujenzi, anasema Esther.

" Kabla ya mradi watoto 1,300 walikosa nafasi, lakini baada ya mradi awamu ya kwanza waliandikishwa 320, ya pili 533 na ya tatu 450, aidha tulikuwa na idadi kubwa ya walioshindwa kumudu KKK takribani 1,850 lakini kwa sasa tatizo limeisha kwenye maeneo ya mradi," amesema Esther.

Yusuph Singo, Ofisa Elimu kutoka TAMISEMI anasisitiza kwamba kiwango cha chini cha asilimia 45 cha usajili kilichopo kwenye eneo la mradi kinatia hofu na kinahitaji hatua za haraka , akisisitiza umuhimu wa kushughulikia changamoto hizo na kutambua maeneo mengine nchini yanayokutana na matatizo kama ya Kisarawe, na kutafuta njia bora za kukabiliana nazo.

Singo anasema jitihada hizo zinalenga kuanzisha mazingira salama na ya kirafiki kwa watoto kupata elimu ya awali katika maeneo ambayo fursa hizo hazipo na kwamba kuanzishwa kwa vituo vya utayari vitapelekea kukamilisha ujenzi wa shule kamili za msingi.

ELIMU
NA DK. REUBENI LUMBAGALA



Askofu wa Jimbo Katoliki la Geita, Dk. Flavian Kassala. **PICHA: REDIO MBIU**

MIAKA 2,023 YA IMANI

# Waje viongozi ngangari kama Askofu Kassala kupinga ushoga hadharani

HERI ya mwaka mpya wasomaji na watangazaji wetu, tunaahidi kuwa karibu nanyi na kuwawashia zaidi Mwanga wa Jamii, ndiyo Nipashe.

Tuuanze mwaka kwa kuukemea mmomonyoko wa maadili hasa ndoa za jinsi moja ambayo ni kama 'saratani' inayotishia mustakabali wa kizazi cha sasa na kijacho.

Ni 'gonjwa' lenye athari kiafya, kisaikolojia na kiroho linalostahili kupingwa kwa juhudi zote.

Kukengeuka kwenye ndoa na kupigia debe za jinsi moja zinazohusisha wanawake kwa wanawake au wanaume kwa wanaume, mwaka unapoanza ni janga linaloibua mijadala, hasa unapogusa kanisani Katoliki lenye waamini takribani bilioni 1.3 duniani kote.

Hivi karibuni, ndicho kinachomuibua Askofu Mkuu wa Jimbo Katoliki la Geita, Dk. Flavian Kassala, anayesema hayuko tayari kubarki ndoa ya jinsi moja kwa sababu ni kinyume na maagano ya Mungu ya kutaka binadamu waishi mke na mume na wazaane na kuendeleza vizazi duniani.

Anatoa msimamo wake bila kujali maelekezo au sera za wakuu wa kanisa hilo ambalo linasema linaweza kuruhusiwa Mapadri kubariki uhusiano wa jinsi moja.

Akihubiri katika misa ya Krisimasi kwenye Kanisa la Bikira Maria Malkia wa Amani, huko Geita, anaahidi kuwa hatafanya hivyo, tena ni bora abariki mawe yakajengee nyumba lakini si ndoa ya jinsi moja.

"Binadamu amemuacha Mungu na kufanya mambo yaliyokatazwa, amekataa kuundeleza uumbaji na sasa anafanya mambo yanayomchukiza Mungu, amekuwa akiharibu vizazi kwa kutoa mimba na sasa kubariki na mapenzi ya jinsi moja. Kwangu bora nibariki jiwe lakini sio uchafu huo,"anaonya Askofu Kassala.

Anachosema ni sahihi maana baada ya miaka 2023 ya kuwafundisha waamini Ukatoliki tena kwa mateso makubwa hata wengine wakiuawa mfano Mashahidi wa Imani ya Uganda, huu haukufaa kuwa wakati wa kuzungumza kubariki ndoa za jinsi moja.

Nimpongeze Askofu Kassala ambaye ameamua kuusema msimamo wake waziwazi kwani viongozi wa dini wanao ushawishi mkubwa katika jamii na ndiyo wanaotakiwa kusema hapana kwa sera na melekezo yenye kupotosha yanayotolewa kwa waamini na viongozi wao hata yakitoka kwa mamlaka za juu zaidi.

Kutokana na umuhimu wa viongozi wa dini, ndiyo maana mara kwa mara serikali imekuwa ikiwashirikisha kwenye mipango na mikakati ya nchi ili kurahisisha utekelezaji wake.

Msimamo wa Askofu Kassala unaunga mkono juhudi za wadau zenye lengo la kujenga maadili bora katika nchi hii.

Ni vigumu kupata nchi yenye maadili huku ukiruhusu na kukumbatia ndoa za jinsi moja, ni vyema kusema hapana, kama anavyosisitiza Askofu Kassala kuwa baraka zake atazipeleka kwenye mawe.

Tafsiri nyepesi ya ndoa kuwa ni muunganiko wa mwanaume na mwanamke kama mume na mke, inahusisha jinsi mbili tofauti, wawili hawa wakiungana na kuanzisha familia yao.

Ikumbukwe katika kujenga jamii yenye maadili na mienendo mema, lazima kama taifa kuweka mikakati na misimamo ili kufikia nchi yenye watu wanaoishi kwa maadili.

Serikali kama mdau muhimu katika ujenzi wa maadili kijamii, inashirikisha wengine na taasisi mbalimbali ili kuunganisha nguvu na kufanikisha azma ya kuwa na taifa la watu wenye maadili.

Ndoa za jinsi moja ni suala linalotakiwa kupingwa siku zote, kama taifa Watanzania wanapaswa kuwa na sauti moja kuanzia kwa mwananchi mmoja mmoja, familia, jamii na taifa lote kuzikataa.

Ndoa hizi ziwe zinawahusisha wanawake au wanaume zote si baraka ni za jinsi moja ambazo kuanzia kwenye imani za dini, mila, desturi na tamaduni za nchi hii ni jambo lisilokubalika.

Ni kitu kisichohitaji mjadala mrefu wala kutolewa ufafanuzi kwa vile wengi wanafahamu kuwa hakina nafasi, japo kutokana na ushawishi na msukumo kutoka mataifa ya Magharibi ajenda hiyo inasukumwa na kuhimizwa kupewa nafasi.

Watanzania hawanabudi kuendelea kupaza sauti na kueleza bayana msimamo wa taifa kuwa hawatatoa ruhusu mambo hayo kupandikizwa katika jamii.

Hata katika vitabu vya dini vinaeleza Mwenyezi Mungu ndiye muasisi wa taasisi ya ndoa. Katika kuweka msingi wa ndoa, Mungu aliwaumba Adam (mwanamme) na Hawa (mwanamke), akawabariki, akawaagiza waende wakaitawale dunia na kuzaliana.

Maandiko Matakatifu katika kitabu cha Mwanzo (1:28), Mungu anawabariki na kuwaambia wakazaane, kuongezeka, kuijaza nchi na kuitiisha, ili kutawala viumbe vyote kuanzia samaki wa baharini, na ndege wa angani na kila chenye uhai juu ya nchi.

Kwahiyo, msingi wa Mungu katika suala la ndoa ni mwanamme na mwanamke na katika jinsi hizo mbili tofauti, ndipo kwenye kunakokuwapo na kuzaliana na kuendeleza vizazi.

Kama taifa, Tanzania ina kila sababu ya kulaani na kupaza sauti kukemea ndoa za jinsi moja ili kuendeleza mipango mizuri ya ujenzi wa maadili kwa mustakabali mwema wa nchi na maagizo ya Muumba.

Viongozi wa dini zote, wanaharakati, asasi za kiraia na kila mpenda maendeleo na maadili wanayo nafasi ya kukemea ndoa za jinsi moja kwa 'mdomo mpana' ili msimamo huu ueleweke vyema kuanzia ndani ya nchi hadi nje ya mipaka.

Mwaka 2011, Waziri Mkuu wa Uingereza David Cameron, alitishia kuwa nchi yake inapanga kusitisha misaada kwa taifa ambalo sheria na katiba zao, hazitambui mashoga na ndoa za jinsi moja.

Katika kutoa msimamo wa serikali, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa wa wakati huo, Benard Membe, (marehemu) alisema: "Tanzania ni nchi maskini lakini hatutakubali kuruhusu upuuzi huo eti kwa sababu ya misaada yake na fedha zao, lakini ushoga si utamaduni wetu, hata sheria zetu zinaukataa."

Nikumbushe makanisa na serikali yetu kuendeleza matakwa ya uumbaji na msimamo huo madhubuti uliotolewa 2011 na Wizata ya Mambo ya Nje, zaidi sana, kama nchi iendelee kutumia raslimali zake kikamilifu ili kupitia kupata fedha za kutosha za kuendesha serikali na kuwaletea wananchi maendeleo.

Lazima kutumia juhudi na uzalendo kuepukana na kuitumbukiza nchi katika kadhia na aibu ya kuomba na kutegemea misaada ambayo wakati mwingine inakuja na masharti ya ndoa ya jinsi moja.

Mwandishi ni mwalimu wa Mlali Sekondari iliyoko wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.

**Maoni: +255 620 800 462**

ELIMU
NA GAUDENSIA MNGUMI

# ‘Hata ukikimbia kidogo una faida milioni kiafya’




Milind Soman na Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo.Dk. Damas Ndumbaro, baada ya kukamilisha Marathon ya kilometa 130 kutoka Dar hadi Bagamoyo na kurudi iliyomalizika juzi. **PICHA ZOTE JUMANNE JUMA**

KUKIMBIA mara kwa mara kunapunguza uzito, lakini ni baada ya kurekebisha mlo wako. Kunaboresha afya ya moyo na mfumo wa kinga, kupunguza ukinzani wa insulini kadhalika husaidia mwili kuwa imara zaidi jinsi unavyozeeka.

Ni kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), likisisitiza kufanya mazoezi na kuishi maisha ambayo mwili unashughulishwa (active) muda wote.

Kukimbia ni bora zaidi inasema WHO kwa vile kunaondoa ukinzani wa insulini, ikimaanisha kuwa hiki ni kichocheo kinachosafirisha sukari kwenye viungo vyote mwilini, hivyo kukosa mazoezi kunasababisha mwili kujenga mazingira yakuizuia insulini isifanye kazi kiufanisi.

Kukwama huko, kutasababisha kisukari ambavyo ni matokeo ya ukinzani, hivyo mazoezi hurahisisha kazi ya insulini kwa sababu sukari inatumika kikamilifu na kuufanya mwili kuwa na hali bora zaidi.

Mwanariadha mashuhuri nchini India,Milind Soman, yuko nchini akisisitiza umuhimu wa mazoezi hasa kukimbia, akiwahamasisha Watanzania kufanya hivyo ili kujenga afya ya mwili kwa watu wa rika zote.

> “Kukimbia huweka mwili sawa, timamu na kujiepusha na magonjwa yasiyoambukiza.. Lakini ili kuwa na afya njema ni muhimu kulala inavyotakiwa, kufanya mazoezi, kula mlo bora na mwepesi , kutumia vyakula vya asili, visivyosindikwa, kukobolewa, wala kuchakatwa viwandani na kujua namna bora ya kukabiliana na msongo wa mawazo (stress).”




Akiwa jijini Dar es Salaam, anazungumza na wanahabari akisema amekuja kushiriki mbio za ‘ultra Marathon’ zinazohusisha kutembea na kukimbia umbali mrefu zaidi wa marathon iliyozoeleka kisheria ambayo ni kilomita 42.

Anawaambia wanahabari kuwa ameanza kukimbia mbio hizo akiwa na miaka 30 na kwamba mazoezi ni afya kwa vile yanaondoka mambo yasiyohitaji au yanayoweza kuumiza mwili.

Amemaliza mwaka 2023, akifanya mbio za kilometa 130 kutoka Dar es Salaam hadi Bagamoyo kwenda na kurudi mazoezi yaliyokamilika juzi Jumapili yakianza Jumamosi Desemba 30, kwa lengo la kujenga afya wala si kushindana ili kupata medali za fedha au dhahabu na kuweka rekodi za kimataifa, kama wengi wanavyodhani.

Soman anapozungumza na wanahabari kwenye Ubalozi wa India, anasema Marathon ya Tanzania inaandaliwa kwa ushirikiano wa Ubalozi wa India na Shirikisho la Riadha Tanzania (RT).

Anataka Watanzania, familia, jamii kuhamasishana kushirikiana kuanzisha ultra Marathon, inayounganisha watu na kujenga afya bora ya jamii, ambayo kila mmoja anakimbia na kutembea, mfano familia yake nzima mama na mkewe wanashiriki.

“Kukimbia huweka mwili sawa, timamu na kujiepusha na magonjwa yasiyoambukiza.. Lakini ili kuwa na afya njema ni muhimu kulala inavyotakiwa, kufanya mazoezi, kula mlo bora na mwepesi , kutumia vyakula vya asili, visivyosindikwa, kukobolewa, wala kuchakatwa viwandani na kujua namna bora ya kukabiliana na msongo wa mawazo (stress).”

Mwanaridha huyu anatangaza ujumbe wa watu kufanya maisha yao yawe ya kimazoezi na kujishughulisha badala ya kukaa na kubweteka.

Anasema haendi kwenye vituo vya mazoezi ‘jim’, anafanya mazoezi nyumbani hasa kutembea na kukimbia umbali mrefu yeye pamoja na jamii au watu anaoishi nao.

**SOMO LINAWEZEKANA**

Katika mazungumzo yake Soman, ana ujumbe kuwa maisha ya kupumzika kutumia simu muda wote, kuchati, kupenda kulala zaidi na kula vyakula vingi hasa vya kukaanga na mafuta mengi hakusaidii badala yake ni kuuchosha mwili.

Mathalani, WHO inasema mazoezi yanashusha lehemu au ‘kolestro’ mwili na kwa ujumla huondoa vitu visivyokuwa na faida ambavyo vimewekwa akiba mwilini kama mafuta, chumvi na sukari ambavyo hujikusanya kwenye damu au ndani ya viungo.

WHO inaeleza kuwa ukifanya mazoezi moyo unakuwa na ufanisi unakwenda mbio, mapafu yanafanya kazi ya ziada, chumvi, sukari na mafuta yanayojibanza kwenye mishipa vinavunjwa vunjwa na kuondoshwa huku insulini inakuwa na kazi nyepesi, hivyo mwili kuimarika.

**SAFARI YA KUBADILIKA**

Ujumbe wa nyota huyo wa India ambaye pia ni mcheza sinema anayesema licha ya kucheza filamu hakai chini na kutazama kwa sababu anapenda kujishughulisha muda wote, anahimiza kuushughulisha mwili na hivyo kuishi maisha ya mazoezi na shughuli zaidi.

Ukiangalia kile anachosema ni kubadilisha mifumo ya maisha hasa kwa wanaokaa mijini, wapendelee kutembea na kuachana na bodaboda.

Wafanyakazi walioko ghofani wasipendelee kupanda lifti, panda na shuka kwa miguu ni muhimu.

Unapopanda daladala usishuke kwenye kituo mahususi teremka viwili au kimoja kabla tembea ili kuupa mwili mazoezi yanayokutoa jasho siyo kukwepa kutembea kama wengi wanavyofanya.

Zama hizi zina maradhi mengi na hasa yasiyoambukiza kama kisukari, figo, uzito kupindukia, saratani na moyo, japo yatahitaji dawa na kuwaona wataalamu, mazoezi na michezo pia ni tiba isiyo na gharama.



# 'Wajane msikimbilie kuolewa, leeni familia'

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

WAJANE wametakiwa kuacha kukimbilia kuolewa na wanaume wengine ili waweze kuangalia ustawi wa familia kwanza kwa kuwapatia watoto wao elimu na mambo muhimu kwenye maisha.

Hayo yalisemwa na mlezi wa wajane wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Ashura Kimwaga wakati wa mkutano wa wanachama wa Chama cha Wajane wa Kata ya Nkuhungu.

Kimwaga, alisema wajane wengi wamekuwa wakikimbilia kuolewa baada ya kufiwa na waume zao na kuwaacha watoto wakihangaika.

"Ukifiwa katika umri mdogo unaweza kuolewa, lakini wale wenye umri kama wangu tulia ulee watoto na wajukuu, wengi wamepoteza mali walizokuwa nao kwa sababu ya kuingia kwenye ndoa na mahusiano yasiyo sahihi na kupelekea kile alichoachiwa kwa ajili ya familia kupotea "," alisema

Aliwataka wanachama wa chama hicho kushikamana ili fedha zitakazopatikana kutokana na michango yao na wadau wengine kutumika kama mtaji wa kuanzisha miradi ya ujasiriamali na kujikwamua kiuchumi.

Alisema chama hicho ambacho kilianzishwa Oktoba mwaka 2022 kikiwa na wanachama 102 hadi sasa kina wanachama 284.

Alisema kuwa changamoto kubwa wanayokabiliana nayo ni baadhi ya wajane kutokuwa na uwezo wa kulea familia, kusomesha watoto, kudhulumiwa mali zao, kutengwa na kunyanyaswa.

"Wengine wamejiingiza kwenye mikopo kausha damu, hivyo kupelekea kuchukuliwa vitu vya ndani," alisema.

Alisema chama hicho kinaundwa na mitaa saba ya Bochela, Itega, Salala, Mnyakongo, Amani, Muungano na Mtube.

Mgeni rasmi katika mkutano huo ambaye ni Mwenyekiti wa Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi Tanzania Mkoa wa Dodoma, Mary Mabhaya, alisema wajane hao wataunda vikundi za ujasiriamali na kupatiwa elimu ya kutengeneza bidhaa zenye ubora.

Alisema miradi hiyo itawawezesha kuwa na uhakika wa kipato na kuinua uchumi wao na familia zao.

Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) wa Chama cha Mapinduzi (CCM) Kata ya Nkuhungu, Mahija Mataka aliwataka wanachama hao kuacha uchoyo katika kuambiana fursa ili kuinuana kiuchumi

Diwani wa Viti Maalum Kata ya Nkuhungu, Rose Nitwa aliwataka kuendelea kujiamini na kujishughulisha na kazi mbalimbali ili kuongeza vipato vya familia.

Alisema wamekuwa wakitoa misaada mbalimbali kwa wahitaji wakiwamo wajane ili kuwapunguzia hali ngumu ya maisha.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Bochela, Julius Macheya alisema ni muhimu wajane kujiunga kwenye vikundi hali itakayosaidia kujiinua kiuchumi.

## Watoto 19 wazaliwa mwaka mpya

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

WATOTO 19 wamezaliwa katika Hospitali ya Rufani Mkoa wa Dodoma wakati wa mkesha wa mwaka mpya wa 2024

Ofisa Muuguzi wa kinamama wa hospitali hiyo, Juma Masoud alisema kuwa watoto hao waliozaliwa katika kipindi cha saa 24 ni 19 na mama zao, wanaendelea vizuri.

"Tunashukuru Mungu tumepata watoto bila vifo ndani ya mwaka mpya kwa sababu wote na wazazi wao wanaendelea vizuri," alisema Masoud.

Aliishukuru Wizara ya Afya kwa kupeleka vifaa kwenye hospitali hiyo kwa kuwa vinasaidia kutoa huduma haraka kwa wajawazito wakati wa kujifungua na watoto wao.

Alisema serikali inaijali sekta ya afya, hivyo jamii isite kujitokeza kupata matibabu katika hospitali hiyo.

Aliwahimiza wajawazito kuhudhuria kliniki ili waweze kujifungua salama.



**"Tunashukuru Mungu tumepata watoto bila vifo ndani ya mwaka mpya kwa sababu wote na wazazi wao wanaendelea vizuri," alisema Masoud.**



Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, (kulia) akikabidhi zawadi mbalimbali kwa Mkuu wa kituo cha kulelea watoto yatima cha Malaika wa Matumaini,Sista Frola Phaustine kilichopo Manispaa ya Singida zawadi ambazo zimetolewa na Rais Samia Suluhu Hassan kwa vituo viwili, kingine ni Amani Center for Street Children. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Watanzania watakiwa kumuunga mkono Samia

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

WATANZANIA wametakiwa kumuunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan kusaidia vituo vya watoto yatima na wanaoishi katika mazingira magumu ili nao wajihisi kama watoto wengine nchini.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba wakati akikabidhi vyakula kwa vituo vya kulelea watoto yatima na waishio katika mazingira magumu vya Malaika wa Matumaini na Amani Center for street Children vilivyopo Halmashauri ya Manispaa ya Singida kwa ajili ya kusheherekea mwaka mpya wa 2024.

Vituo hivyo vimekabidhiwa mchele, mbuzi, maharage, sukari, sabuni, unga wa sembe na mafuta ya alizeti na Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba kwa niba ya Rais Samia.

Serukamba, alisema ni dhamira ya dhati ya rais kungana na watoto yatima na waishio katika mazingira magumu mkoani Singida kusherehekea mwaka mpya huo baada kuuaga 2023.

"Nipende kuwapongeza na kuwashukuru masista pamoja na wadau wengine ndani ya Mkoa wa Singida kwa jitihada zao katika kuyahudumia makundi yenye uhitaji, juhudi hizi zinadhihirisha wazi kuwa wadau na jamii kwa ujumla wanavyounga mkono juhudi za serikali kuhakikisha makundi hayo yanapata afya, elimu, chakula, mavazi na malazi, " alisema.

Serukamba alitoa wito kwa wadau na jamii ndani na nje ya Mkoa wa Singida kuungana na Rais Samia kuendelea kuwakumbuka wenye uhitaji wakati wote.

Diwani wa Kata ya Minga, Ibrahimu Mrua na Taasisi ya Uweza wa Bwana wametoa mchele, sabuni, mafuta, unga wa sembe na ngano na maharage kwa Kituo cha Malaika wa Matumaini.

Mrua, alisema wametoa msaada huo kwa kutambua kuwa kusaidia wenye mahitaji kunaleta faraja kwao na neema na kutoa wito kwa watu wengine kuwakumbuka watoto yatima na wanaoishi katika mazingira magumu.

Mkuu wa Kituo cha Malaika wa Tumaini, Sista Frola Phaustine, alimshukru Rais Samia kwa msaada huo na kusema ameonyesha dhahiri upendo wa dhati kwa yatima.

Phaustine alisema kituo hicho kinakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa mabweni ya kutosha kwa watoto wanaofikia umri mkubwa na kuiomba serikali isaidie kutatua changamoto hiyo.

Kituo cha Malaika wa Matumaini kina watoto yatima 48 ambao wamekuwa wakipatiwa elimu kutokana na kuwa na shule ya awali, msingi na sekondari ambayo itaanza mwaka huu.





# Malori yenye shehena ya soya yazuiwa kuingia nchini

- Madereva walia ukata, wahofia kufa njaa

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

ZAIDI ya malori 40 yenye shehena ya mashudu ya soya kutoka nchini Malawi yamezuiwa kuingia nchini kwa zaidi ya wiki mbili katika mpaka wa Kasumulu wilayani Kyela Mkoa wa Mbeya kutokana na serikali ya Tanzania kuzuia soya na mazao yake kuingia nchini kwa kuhofia kusambaa kwa virusi.

Serikali ya Tanzania kupitia Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu (TPHPA) imezuia bidhaa hizo kwa madai kuwa nchi hiyo imebainika kuwa na virusi hatari vinavyoweza kuhatarisha uzalishaji wa soya nchini.

Wakizungumza na wandishi wa habari juzi madereva wa malori hayo waliiomba Serikali kuwasaidia kwa sababu hawajui hatima yao tangu wamekwama kwenye eneo hilo.

Mmoja wa madereva hao, Swalehe Yusuph alisema tatizo hilo limewakumba zaidi ya watu 80 wanaofanya kazi kwenye malori hayo, kila lori lina wafanyakazi wawili, dereva na utingo.

Alisema tangu wamekwama kwenye eneo hilo wameishiwa hata fedha za matumizi kutokana na kukaa muda mrefu kwenye eneo hilo.

"Tunaiomba Serikali ituangalie na sisi kama binadamu kwa sababu tangu tumekwama hapa hatujui cha kufanya, tunaomba tusaidiwe ili tatizo hili liishe na tuendelee na safari," alisema Yusuph.

Meshack Mwakipesile alisema alipofika mpakani alizuiwa kuendelea na safari na kutakiwa kupeleka gari kwenye eneo la maegesho.

Alisema alipohoji sababu za kuzuiliwa alijibiwa mzigo una virusi ambavyo ni hatari endapo vitasambaa nchini.

Alisema kutokana na hali ngumu ya maisha, wanalazimika kulala kwenye magari hayo huku wakihofia afya zao kwa njaa kwa sababu hawana fedha kwa ajili ya kununulia chakula na mahitaji mengine.

"Serikali inasema mzigo huu una madhara, sasa tunajiuliza inamaanisha sisi ambao tunalala kwenye haya magari hatuwezi kupata madhara na inatuangaliaje sisi?" Alihoji Mwakipesile.

Kisingi Shaaban alimuomba Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe kuwasaidia kumaliza tatizo hilo kwa kuamuru mzigo ushushwe ili waendelee na safari badala ya kuuzuia kwenye magari.

Shaaban alisema kwenye mipaka mingine mzigo ambao hautakiwi kuingia kwenye nchi husika, inaamriwa kushushwa na kupelekwa kwenye maghala na si magari.

Nipashe lilifanikiwa kuiona barua ya TPHPA ambayo imesainiwa na Mkurugenzi Mkuu wake, Profesa Joseph Ndunguru ikisisitiza mizigo hiyo kutoruhusiwa kuingia nchini.

Akizungumza kwa njia ya simu, Profesa Ndunguru alithibitisha kutoa zuio hilo na kwamba kwa sasa wanaendelea kufanya tathimini ya virusi hivyo nchini Malawi.

Alisema tathimini hiyo ikikamilika ndipo wataamua kuruhusu mashudu hayo kuingia nchini au la na kuwataka madereva waliokwama kuendelea kuwa watulivu..




Msemaji wa Jeshi la Polisi SACP, David Misime akikagua matumizi ya mifumo mbalimbali ya kidijitali ambayo kwa sasa imeanza kutumika ndani ya Jeshi la Polisi na kuleta ufanisi zaidi katika utekelezaji wa kazi za Jeshi la Polisi alipotembelea mkoa wa Songwe. **PICHA: ISSA MWADANGALA**

## Udumavu wamtisha DC Makete

**Na Elizabeth John,** MAKETE

MKUU wa Wilaya ya Makete Mkoa wa Njombe, Juma Sweda ametoa rai kwa wakazi wa wilayani hapa kuungana katika kampeni ya kutokomeza udumavu.



Rai hiyo imetolewa wakati wa Mkutano Mkuu wa Chama cha Maendeleo Makete (MDA) uliofanyika wilayani hapa.

Sweda alisema Njombe ni moja ya mikoa nchini inayokabiliwa na changamoto ya udumavu hivyo ipo haja ya hatua za makusudi kuchukuliwa kutokomeza tatizo hizo ambalo ni janga kwao.

"Suala la lishe bora ni changamoto inabidi watu wajue sababu ya udumavu ni kuanzia mtoto miaka sifuri ndiyo tatizo linakuwa kubwa sana, unakuta mtu haelewi analalamika kumbe ni udumavu, alisema Sweda.

Alisema kama jamii haitapambana na udumavu kwa watoto kuanzia mwaka hao hadi miaka mitano kutakuwa na kizazi kilichodumaa moja kwa moja na hata mwanamke atakuwa na nafasi kubwa ya kutazaa mtoto mwenye tatizo hilo.

Sweda alisema wakati umefika kwa wakazi wa Makete waliopo nje kurudi na kufanya mageuzi katika uwekezaji kwenye sekta za kilimo, majengo na utalii katika Hifadhi ya Kitulo.

Awali Mwenyekiti wa Chama Cha Maendeleo Makete (MDA), Clement Sanga alisema chama hicho kipo tayari kuunga mkono jitihada za wilaya za kutokomeza udumavu kwa kutoa ng'ombe wa maziwa shuleni.

"Hiki ni chama cha hiyari kwa ajili ya kujiletea maendeleo katika wilaya yetu hasa jamii ya Wanamakete ambao wako nje," alisema Sanga.

# Ajali yajeruhi watano lori likigonga magari manne

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATU watano wamejeruhiwa mkoani hapa baada ya lori lenye shehena inayosafirishwa kwenda Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) kufeli breki na kuyagonga magari mengine manne yakiwemo mawili ya abiria aina ya Toyota Hiace yanayofanya safari kati ya Jiji la Mbeya na mji mdogo wa Mbalizi.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Benjamin Kuzaga alisema kuwa ajali hiyo ilitokea juzi asubuhi kwenye eneo la mteremko.

Alisema lori hilo lenye namba za usajili T.428 DXD na tela T.860 BWM aina ya FAW lilizigonga Hiace hizo T.287 DGK na T.977 DBN zinazofanya safari kati ya stendi kuu ya mabasi ya jijini Mbeya na mji wa Mbalizi.

Aliyataja magari mengine katika ajali hiyo kuwa ni aina ya Sienta T.163 DDA na lori lingine aina ya Howo T.595 ECU lenye tela T.336 ECS.

Aliwataja majeruhi wa ajali hiyo kuwa ni Neema Mwakisambe (23), Mkazi wa Nzovwe, Selina Ngonyani (31), wa Sokomatola, Tunazael Elikunda (58), wa Ghana, Upendo Sembalakane (54), wa Sokomatola na Steven Sinkwembe (40), wa Iwambi ambaye ni mmoja wa madereva wa daladala hizo.

Alisema ajali hiyo pia ilisababisha uharibifu wa magari yote sita na mali zilizokuwa zimebebwa.

Alisema chanzo cha ajali hiyo ni uzembe wa dereva wa lori hilo kutokana na kushindwa kulimudu katika eneo lenye mteremko baada ya kufeli breki.

"Tunaendelea kumsaka dereva wa lori hilo ambaye ametambuliwa kwa jina la Msafiri Mwawila kwani alikimbia na kutokomea kusikojulikana baada ya kusababisha ajali hiyo," alisema Kamanda Kuzaga.

Alisema majeruhi wa ajali hiyo wanaendelea kupatiwa matibabu katika Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya huku hali zao zikiendelea vizuri.

Kamanda huyo alisema wanaendelea kumtafuta mmiliki wa lori hilo ili kuhamisha seheba ya mzigo uliokuwa umebebwa na kuwasadia kumpata dereva wake.

Alisema polisi wameimarisha ulinzi kwenye eneo la ajali ili kuhakikisha mzigo huo unakuwa salama mpaka utakapokuwa umehamishiwa kwenye gari lingine na kusafirishwa kwenda DRC ambako ulikuwa unapelekwa..



## Tume ya Utangazaji Zanzibar yapewa somo

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

TUME ya Utangazaji Zanzibar imetakiwa kuimarisha mabadiliko zaidi ya kiutendaji katika usimamizi wa utangazaji kabla ya kufanyika kwa Uchaguzi Mkuu mwakani.

Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Suleiman Ame Khamis alisema kuwa kazi kubwa inayotakiwa kusimamiwa na tume hiyo ni kufanya tathmini mwaka huu ili kuendelea kufanya kazi zao kwa mujibu wa sheria, kanuni na miongozo.

Khamis aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na wafanyakazi na uongozi wa tume hiyo katika kikao kilichofanyika Ukumbi wa Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale Kikwajuni Mjini Unguja.

Aliwataka watendaji wa tume hiyo kufahamu kuwa ifikapo mwaka 2025 Uchaguzi Mkuu unatarajiwa kufanyika, hivyo tume hiyo inahusika kwa asilimia kubwa kusimamia vyombo vya habari ambavyo ndio vinatumiwa na wanasiasa kutangaza sera zao.

"Nafasi yetu sisi tume katika uchaguzi ni jukumu letu kusimamia vyombo vya habari tulivyovisajili ni lazima kutumia ujuzi na taaluma kwa uadilifu na umakini," alisema mwenyekiti huyo.

Alisema kufanya hivyo kutasaidia kuijengea sifa zaidi tume hiyo na kimabadiliko,iwapo itashindwa kufanya hivyo wataiangusha serikali katika kusimamia sekta ya utangazaji.

Katibu Mtendaji wa tume hiyo, Suleiman Abdulla Salim, alisema itaendelea kufanya kazi kwa ushirikiano kwa mujibu wa sheria na miongozo na kanuni zake.

"Katika usimamizi wetu hasa wa vyombo vya habari tutajipanga zaidi ili mwaka 2024 iwe bora katika utendaji wa kazi zetu," alisema.

# Mwinyi ataka usafiri wa treni urejee Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk Hussein Ali Mwinyi amesema kuna haja kurejesha usafiri wa treni visiwani hapa.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana wakati akiweka jiwe la msingi katika kituo cha kisasa cha mabasi kinachojengwa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) eneo la Kijangwani mjini Unguja.

Alisema historia inaonyesha kuwa kipindi cha ukoloni kabla ya kufanyika kwa Mapinduzi ya Zanzibar mwaka 1964, kulikuwa na usafiri wa treni hivyo ni vyema kurejesha historia hiyo.

Akizungumzia kuhusu ujenzi wa kituo hicho, alisema eneo hilo ni makutano ya wananchi kusubiri usafiri, hivyo umefika wakati wa kuwa na utaratibu mzuri wa miundombinu ya usafiri wa kutenga maeneo maalumu ya kuwasili na kuondoka mabasi kama zilivyo nchi nyingine duniani.

Alisema Zanzibar ni sehemu ya Dunia, hivyo umefika wakati kuwa na vituo vya kisasa vya mabasi na maegesho ya magari ili mji wa Zanzibar uwe na mandhari nzuri.

Dk. Mwinyi aliitaka ZSSF kujenga kituo kingine cha mabasi katika Hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja ili usafiri wa umma uwe na utaratibu mzuri wa kuingia kutoka mjini na kuondoa msongamano wa daladala kando ya barabara.

Alisema miradi inayojengwa na ZSSF itaongeza pato la mfuko huo na imani kwa wananchi kuwa fedha zao zipo sehemu salama.

Mkurugenzi wa ZSSF, Nassor Shaaban Ameir, alisema mradi huo una lengo la kuisaidia jamii kukuza kipato cha kila siku na kuboresha huduma za jamii.

Kwa mujibu wa Ameir, mradi huo unatarajiwa kurudisha fedha za uwekezaji za ZSSF kwa kipindi cha miaka saba ijayo.

Alisema kituo hicho ambacho kitakuwa na uwezo wa kuegesha mabasi 80 kwa wakati mmoja, ujenzi wake utagharimu Shilingi bilioni 8.6 hadi kukamilika .

Alisema mkandarasi wamemlipa Shilingi bilioni 3.05 kwa ajili ya ujenzi huo ambao ulianza Mei, mwaka jana na unatarajiwa kukamilika Machi mwaka huu.

Ameir alisema katika kituo itawekwa mitambo ya ulinzi na usalama, kutakuwa na maduka, ofisi binafsi na huduma nyingine muhimu za kijamii.



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla (kushoto) akisalimiana na Meneja wa Biashara Zanzibar wa Benki ya NMB, Naima Said Shaame (kulia) muda mfupi kabla ya kuanza kwa matembezi ya hisani katika tamasha la mazoezi ya viungo kitaifa. Matembezi hayo yalianzia mnara wa Mapinduzi Michenzani mpaka katika uwanja wa Amani visiwani huko. Katikati ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji wa Serikali ya Zanzibar, Mudrik Soraga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watakiwa kutunza matunda ya Mapinduzi

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Dk. Khalid Salum Mohamed amewataka wananchi visiwani hapa kutunza matunda ya Mapinduzi ili kuwa endelevu kwa faida yao na taifa kwa ujumla.

Akizungumza jana wakati wa hafla ya uwekaji wa jiwe la msingi katika Soko la Wananchi wa Mkwajuni Mkoa wa Kaskazini Unguja, alisema matunda hayo yanahitaji kulindwa kwa maslahi ya wananchi.

Mohamed alisema ni wajibu wa kila mwananchi kutunza miradi hiyo ya maendeleo ili idumu kwa muda mrefu na kuwasaidia kujikwamua na hali ngumu ya maisha.

Aliwataka wakulima, wafugaji na wavuvi kuzitumia nyenzo za uzalishaji wa mazao na kupata mazao bora na kusaidia vijana kupata ajira.

Alisema ushirikiano ni muhimu katika nchi ili kuweza kusonga mbele kwa maendeleo na kuwa na Taifa imara.

"Kabla ya Mapinduzi watu walikuwa wanaishi kwa matabaka , hivyo Mapinduzi yamekuja kuondoa matabaka hayo na kupiga hatua ya maendeleo, " alisema.

Akitoa taarifa za ujenzi wa soko hilo, Katibu Mkuu Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), Issa Mahfoudh Haji, alisema likikamilika litatumika kwa biashara mbalimbali, ikiwemo mnada wa mazao.

Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Rashid Hadid Rashid, aliwataka wananchi kulitumia vizuri soko hilo na kuacha kufanya biashara katika mazingira yasiyo rasmi.

Ujenzi wa soko hilo ulianza Machi mwaka jana na unatarajiwa kukamilika Mei mwaka huu na kwamba zaidi ya Shilingi milioni 300 zimetumika katika hatua iliyofikia.

# HABARIPICHANI



Waumini wa Kanisa la Kambi ya Waebrania lililoko Kimara Suka, Jijini Dar es Salaam, wakipeana mkono wa heri katika mkesha wa kuupokea mwaka mpya wa 2024 usiku wa kuamkia jana **PICHA: IMANI NATHANIEL**



RAIS wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi akimsikiliza Mhandishi wa Kampuni ya M+M Architects Co.Ltd Ismail Burhani Mvungi, akitoa maelezo ya michoro ya majengo ya Kituo cha Mabasi Kijangwani wilaya ya Mjini Unguja, wakati wa hafla ya uwekaji wa jiwe la msingi la ujenzi huo. **PICHA: IKULU**



Waumini wa Kanisa la Romani Katoliki Kristo Mfufuka, wilayani Muheza mkoani Tanga wakiendelea na ibada ya kuukaribisha mwaka mpya wa 2024, jana kanisani hapo mtaa wa Majengo shimoni ambayo iliendeshwa na Padri wa kanisa hilo, Martine Kihiyo. **PICHA: STEVEN WILLIAM**



Waumini wa Kanisa la Romani Katoliki Kristo Mfufuka, wilayani Muheza mkoani Tanga wakiendelea na ibada ya kuukaribisha mwaka mpya wa 2024 jana kanisani hapo mtaa wa Majengo shimoni ambayo iliendeshwa na Padri wa kanisa hilo Martine Kihiyo. **PICHA: STEVEN WILLIAM**



Viongozi wa dini kutoka madhehebu mbalimbali wilayani Bukombe mkoani Geita pamoja na Wazee wa wilaya hiyo wakimsikiliza Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko (hayupo pichani) katika mkutano uliolenga kubadilishana mawazo na kumshukuru Mungu kwa mwaka 2023.**PICHA:MPIGAPICHA WETU.**



Meneja wa Shule ya Paradise Mission iliyopo Mbalizi mkoani Mbeya (wapili kulia) akimkabidhi msaada wa vitu mbalimbali mmoja wa wakazi wa kata ya Lwanjilo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya hivi karibuni. Mkazi huyo ni miongoni mwa wazee 300 walionufaika na msaada huo. **PICHA: NEBART MSOKWA.**

# Tsunami yaipiga Japan

**TOYAMA,** JAPAN

NYUMBA takribani 33,500 zimekosa huduma ya umeme katika eneo ambalo limepigwa na mfululizo wa matetemeko makubwa ya chini ya bahari nchini Japan, ambayo athari zake zimeshuhudiwa hadi kwenye miji ya mashariki ya mbali ya Russia.

Mamlaka ya Hali ya Hewa ya Japan ilisema kuwa tetemeko hilo lililotokea jana, lilikuwa na ukubwa wa 7.6 kwa kipimo cha Richter na miji iliyoathirika zaidi ni Toyama, Ishikawa na Niigata, ambayo inapatikana kwenye kisiwa kikubwa cha Honshu katika mwambao wa magharibi wa Bahari ya Japan.

Shirika la habari la Russia, TASS, limewanukuu mameya wa miji ya Vladivostok na Nakhodka wakitangaza tahadhari ya tsunami katika maeneo hayo yaliyo kwenye kisiwa cha Sakhalin.

Mamlaka ya Hali ya Hewa ya Japan iliripoti matetemeko kwenye mwambao wa Ishikawa na maeneo yake ya karibu jana saa 10:00 jioni

Hata hivyo serikali ya Japan imeanzisha kituo maalum cha dharura kukusanya taarifa za matetemeko na tsunami na kuzisambaza haraka kwa raia, kwa mujibu wa Waziri Mkuu Fumio Kishida, aliyerejelea onyo la kuhama haraka katika maeneo yaliyoathirika.

**DW**

# Rais Tshisekedi amwagiwa pongezi za ushindi

**KINSHASA,** DRC

JAMII ya kimataifa imeendelea kutuma ujumbe wa pongezi kwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) kufuatia ushindi wa Rais Felix Tshisekedi kwenye uchaguzi mkuu wa Desemba 20, 2023.

Kiongozi wa Umoja wa Afrika na Rais wa Comoros Azali Assoumani alikuwa miongoni mwa viongozi wa kwanza kumpongeza Rais Tshisekedi kwa ushindi wake wa asilimia 73.34 ya kura zilizopigwa katika uchaguzi mkuu.

Katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) ujumbe wa heri njema kutoka Tanzania, umetumwa Kinshasa huku Rais Samia Suluhu Hassan pia akichapisha salamu zake kwenye mtandano wa kijamii wa X.

"Nina matumaini kwamba tutaendelea kufanya kazi kwa karibu na kuboresha uhusiano kati ya mataifa yetu mawili,' alisema Rais Samia.

Pia Rais wa Burundi, Evariste Ndayishimiye, alituma ujumbe wake wa heri njema kupitia mtandao wa kijamii wa X na kuomba amani kudumu baada ya ushindi huo kutangazwa.

Katika ujumbe wake, kiongozi huyo wa zamani wa jumuiya ya EAC alisisitiza wote wenye kupinga matokeo yaliyotangazwa, kuwasilisha kesi mbele ya mahakama kupitia njia zinazofuata muongozo wa sheria.

Kiongozi wa upinzani nchini Kenya Raila Odinga naye, amemtakia Rais Tshisekedi kila la kheri anapoanza muhula wake wa pili madarakani.

"Ninamuombea uongozi wake ulete mabadiliko mema na mafanikio katika taifa hilo. Nawatakia raia wa DRC kila la kheri katika juhudi zao kujiinua upya, kuidhibiti na kuendeleza taifa lao," alisema Odinga.

Tshisekedi alishinda uchaguzi huo ulioandaliwa Desemba 20, 2023 kwa kura zaidi ya milioni 13 ambazo ni asilimia 73 ya jumla ya kura zilizopigwa katika uchaguzi huo. Mpinzani wake wa karibu alikuwa Moise Katumbi aliyepata kura milioni 3 ambazo ni asilimia 18 ya kura zilizopigwa huku Martin Fayulu akiibuka nambari tatu kwa kura laki tisa ambazo ni asilimia tano ya kura zote zilizopigwa.

Tshisekedi alikuwa anakabiliana na wagombea 19, akiwemo mmoja wa kike, Ifoku Marie-Josee Mputa Mpunga ambaye amekubali kushindwa na kumpa kongole mshindani, Rais Tshisekedi.

Katika taarifa iliyochapishwa kwenye ukurasa wake wa mtandao wa kijamii wa X, Marie alisema kwamba, "ushindi wake Tshisekedi unaonyesha imani ya raia wa DRC katika uongozi wake".

Kiongozi wa upinzani nchini Ufaransa, Marine Le Pen, mbali na kutuma ujumbe wa heri njema na kumpongeza Rais Tshisekedi, pia alisema "Ninawatumia raia wa DRC heri njema na dua ya amani.

Hasa wanaokabiliwa na vita ambavyo vinasahaulika katika jimbo la Kivu, Ufaransa ni sharti isimame na taifa hilo".

Rais wa Afrika Kusini Cyril Ramaphosa katika ujumbe wake wa kumpongeza Rais Tshisekedi, aliwapongeza raia wa DRC kwa kuwa watulivu na kuonyesha umoja wakati walipo subiri matokeo rasmi kutangazwa.

"Ninaomba utulivu hasa ikiwa kunaye kiongozi ambaye atapinga matokeo haya na kuwataka wote kutumia njia za kisheria kulingana na katiba ya nchi hiyo kuwasilisha malalamishi yao rasmi,' alisema Rais Ramaphosa.

Rais mstaafu wa Kenya Uhuru Kenyatta, naye alituma ujumbe kupitia mtandao wa X ukimpongeza Rais Tshisekedi, huku akishauri yeyote kuwasilisha malalamiko yake kupitia njia za Mahakama huku akitaka amani idumu katika eneo la mashariki mwa DRC.

Katika ujumbe wake wa mwisho wa mwaka Rais wa Rwanda Paul Kagame, aliomba kuwa na hali ya usalama katika taifa jirani na kusema kwamba Rwanda inatizama suala hilo kwa uangalifu. **BB**



Rais Felix Tshisekedi wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC). **PICHA: MTANDAO.**

# Russia yawahukumu wapiganaji 200 wa Ukraine

**MOSCOW,** RUSSIA

WAZIRI wa Mambo ya Nje wa Russia Sergei Lavrov, amesema Mahakama za taifa hilo zimewahukumu zaidi ya wapiganaji 200 wa Ukraine, kwenda gerezani toka Moscow, kuanza opereshini zake za kijeshi nchini humo.

Lavrov aliyabainisha hayo jana wakati alipofanyiwa mahojiano na shirika la habari la RIA, ambako alieleza kwamba mahakama za nchini kwake zimewahukumu wawakilishi hao 200 wa jeshi la Ukraine, kwa kufanya unyama.

Pande zote zinashutumiana kwa kufanya unyama katika vita ambavyo vimeanzishwa na Russia baada ya kuivamia Ukraine, Februari 2022. Huku Umoja wa Mataifa (UN) ukiendelea kupata ushahidi wa uhalifu wa kivita, na uvunjifu wa haki za binadamu uliofanywa na serekali ya Russia, ikijumuisha mateso, ubakaji, na usafirishaji wa watoto.

Mwezi Machi, mahakama ya kimataifa ya uhalifu ICC ilitoa hati ya kukamatwa kwa Rais wa Russia, Vladimir Putin, kwa usafirishaji wa watoto kuwa umefikia kiwango cha uhalifu wa kivita.

**MASHAMBULIZI**

Licha ya hatua hizo Russia imeendelea kuendesha operesheni zake za kijeshi baada ya kubainisha jana kuwa imeshambulia vituo vya kijeshi katika mji wa Ukraine, Kharkiv na kuharibu majengo ya makazi ya watu, hoteli na vituo vya afya, ikiwa ni kujibu shambulio lililofanywa na Ukraine huko Belgorod.

Msemaji wa Kharkiv alisema, makombora sita yaliyorushwa yamejeruhi watu wasiopungua 28, huku yakifuatiwa na mashambulizi ya ndege zisizo na rubani.

Katika taarifa ya Russia ilisema, shambulio hilo lililoipiga hoteli ya zamani Kharkiv Palace, na makao makuu ya huduma za usalama ya Ukraine limewaua miongoni mwa maofisa wa kijeshi na ujasusi.

Pia ilisema imewauwa na mamluki wa kigeni na wapiganaji waliokua wanajiandaa kufanya uvamizi eneo la mpakani, ambao walihusika katika shambulio la Ukraine dhidi ya Belgorod.

Msemaji wa jeshi wa Ukraine Andriy Yusov,ameviambia vyombo vya habari vya ndani kuwa hakuna kitu chochote cha kijeshi kilicholengwa katika shambulio hilo wala mtu wa kada yake aliyedhurika. **VOA, DW**

HABARI MICHEZO

# KOCHA DODOMA JIJI ASAKA WA KUSAJILI MAPINDUZI CUP

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA mpya wa Dodoma Jiji, Francis Baraza, yupo mjini Zanzibar kwenye Kombe la Mapinduzi kwa ajili ya kusaka wachezaji atakaowaongeza kwenye kikosi chake kipindi hiki cha usajili wa dirisha dogo.

Akizungumza jana kutokea Zanzibar, Baraza ambaye amechukua mikoba ya Melis Medo, amesema amekuwa huko kufuatilia mechi mbalimbali za Kombe la Mapinduzi, huku akiangalia wachezaji ambao anaona anaweza kuwasajili kwenye kikosi chake kwani anaamini kuna vipaji lukuki Zanzibar na hata timu zingine za kigeni zilizoalikwa zinaweza kuwa na wachezaji wenye uwezo mkubwa pia.

"Ndiyo nikiona wale ambao wananifaa na ndiyo mahitaji kwenye kikosi changu, nitawachukua, sitoongeza wengi kwa sababu mara nyingi nikiingia kwenye timu huwa nadili na wale tu ambao nawapata, kwa hiyo ni kuongezea kile ambacho ninacho na kile ambacho wachezaji wanacho ili tuweze kusonga mbele, siwezi kusema kama nitafanya usajili mkubwa sana, ni wawili au watatu tu," alisema Baraza, kocha wa zamani wa Kagera Sugar na Biashara United.

Alisema baada ya kukiangalia kikosi chake kwa muda mfupi, ameona mapungufu upande wa washambuliaji, huku mabeki wake wa kati wakiwa hawana urefu unaohitajika kwenye nafasi hiyo.

"Nilikuwa Kenya, lakini nilikuwa naiona Ligi ya Tanzania, ni ligi bora sana, na hata Dodoma Jiji nilikuwa naitazama siyo timu mbaya, kinachotakiwa ni kuongeza wachezaji wawili watatu, nafasi ambazo naangalia ni ushambuliaji, beki lazima nitaongeza maana nimeona mabeki wangu wa kati pale ni wafupi, unajua ni lazima uangalie pia urefu wa mabeki kwa ajili ya kudili na mipira ya juu," alisema.

Dodoma Jiji inashika nafasi ya saba kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 18 kwa michezo 13 iliyocheza.

KIPAJI...



Mchezaji wa Tenisi, Adam Alli, akipiga mpira wakati wa mazoezi katika viwanja vya Gymkhana jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Azam wazitaka tatu za Vital'O Mapinduzi leo

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

MABINGWA wa kihistoria wa Kombe la Mapinduzi, Azam FC, wamesema mchezo wao wa leo dhidi ya Vital'O ya Burundi ni muhimu kushinda ili kuweka hai matumaini yao kusonga mbele kwenye mashindano hayo yanayoendelea mjini hapa.

Azam FC itashuka dimbani leo majira ya saa 10 alasiri, huo ukiwa ni mchezo wao wa mwisho wa Kundi A, ikiwa ni baada ya mechi mbili ilizocheza ikipata sare moja na kushinda moja.

Akizungumza na waandishi wa habari jana katika Uwanja wa Amaan Sports Complex, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Bruno Ferri, alisema wamejiandaa vizuri zaidi ili kushinda mchezo huo.

Alisema amewaandaa wachezaji wake kwa ajili ya mchezo huo na kuwaelezea juu ya umuhimu wake, ili wacheze kwa ajili ya ushindi.

"Huu mchezo kwetu ni muhimu kushinda, na nimewandaa wachezaji wangu vizuri na kuwapa maelekezo juu ya umuhimu wake," alisema.

Azam FC inaongoza msimamo wa Kundi A ikiwa na pointi nne ikifuatiwa na Vital'O pamoja na Mlandege ambazo kila moja ina alama mbili huku Chipukizi ikiburuza mkia na pointi yake moja.



# Mbeya City yazinduka Championship

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kufanya vibaya katika mechi kadhaa, timu ya Mbeya City juzi ilifunga mwaka 2023 kwa ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Fountain Gate Academy Talents, katika mechi ya kumaliza mzunguko wa kwanza wa Ligi ya Championship, ikichezwa Uwanja wa Sokoine Mbeya.

Lilikuwa ni bao pekee la straika wao tegemeo, Shaaban Maulidi, dakika ya 49 lilioipa faraja timu hiyo iliyoshuka daraja kutoka Ligi Kuu msimu uliopita.

Kwa ushindi huo, Mbeya City inamaliza mzunguko wa kwanza ikiwa na pointi 24, kwenye nafasi ya saba, ikirejesha hai matumaini yake ya kurejea kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao kama itafanya vema mzunguko wa pili wa Ligi ya Championship.

Baada ya kupoteza mechi hiyo, FGA Talents, inakuwa kwenye nafasi ya 14 na pointi zake 12, ikimaliza mechi zake zote 15 za mzunguko wa kwanza.

Mechi nyingine juzi ilichezwa kwenye Uwanja wa Mwadui Complex, wenyeji Stand United wakipata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Pan African ya Dar es Salaam.

Marijani Twalib ndiye aliyeifungia timu hiyo ya Shinyanga bao pekee katika dakika ya sita ya mchezo likiifanya kumaliza mzunguko wa kwanza wa ligi hiyo ikiwa na pointi 22, ikishikilia nafasi ya nane kwenye msimamo. Pan African inabaki nafasi ya 12 ya msimamo ikimaliza mzunguko kwa kwanza na pointi zake 14.

ASidha, wakati mzunguko wa kwanza ya Champoinship ukitamatika, KenGold ya Mbeya inaongoza ikiwa na pointi 35, ikifuatiwa na Mbeya Kwanza yenye pointi 32, Pamba FC ya Mwanza ya tatu na pointi zake 31, Biashara United kutoka Mara iko kwenye nafasi ya nne kwa pointi 30, na TMA ikishika nafasi tano ikiwa na pointi 30 pia.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**CITY YAMNYAKUA ECHEVERRI**

KLABU ya Manchester City imekubali mkataba wa kumsajili kiungo wa kati wa River Plate na Argentina, Claudio Echeverri, kwa mkataba wa miaka sita, na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 17, atabakia katika klabu hiyo ya Amerika Kusini hadi Desemba 2024. **(Fabrizio Romano)**

**VARANE AFUNGULIWA MLANGO**

KLABU ya Manchester United imeamua kutoongeza mkataba wa Raphael Varane kwa miezi 12 zaidi, ikimaanisha kuwa beki huyo wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 30, anaweza kufanya mazungumzo na klabu nyingine kuhusu uhamisho kuanzia jana. **(Mail)**

**CARVALHO ATAKIWA LEICESTER**

LEICESTER City inataka kumsajili winga wa Liverpool, Fabio Carvalho, kwa mkopo baada ya mchezaji huyo wa Kimataifa wa Ureno chini ya umri wa miaka 21, kurudishwa kwa mkopo katika Klabu ya RB Leipzig. **(Sky Sports)**

**OLISE AWANIWA LIVERPOOL**

LIVERPOOL imetuma mawakala kumtazama winga wa zamani wa Ufaransa chini ya umri wa miaka 21, Michael Olise mwenye umri wa miaka 22, mzaliwa wa Crystal Palace, England**. (Football Insider)**

**SARR KUSAINI MKATABA**

KIUNGO wa Tottenham Hotspur na Senegal, Pape Matar Sarr mwenye umri wa miaka 21 - ambaye alipata majeraha wakati wa mchezo wa Jumapili dhidi ya Bournemouth akiwa na tatizo la misuli ya paja - anakaribia kusaini mkataba mpya wa muda mrefu. **(Athletic)**

**KEHRER AKARIBIA MONACO**

KLABU ya Monaco inakaribia kukamilisha usajili wa beki wa Ujerumani, Thilo Kehrer mwenye umri wa miaka 27, kutoka West Ham. **(Fabrizio Romano)**

**LOOKMAN AMULIKWA JUVE**

KLABU za Juventus na Nice na timu kadhaa za Ligi Kuu England zinavutiwa na winga wa Atalanta, Mwingereza Ademola Lookman, 26. **(Mail)**

**KEAN, PATINO KUPISHANA**

JUVENTUS iko tayari kumtoa mshambuliaji wa Italia, Moise Kean mwenye umri wa miaka 23, ili kubadilishana na kiungo wa kati wa Arsenal, Charlie-Michael Patino (20), ambaye yuko Swansea City kwa mkopo. **(Tuttosport)**

**NKETIAH AULIZIWA PALACE**

KLABU ya Crystal Palace imekuwa ikimuulizia mshambuliaji wa Arsenal na Timu ya Taifa ya England, Eddie Nketiah mwenye umri wa miaka 24, kwa nia ya kutaka kumnunua. **(Mail)**

**ARSENAL KUTOA NYOTA**

Kocha wa Arsenal, Mikel Arteta, yuko tayari kuwaruhusu Edie Nketiah, mshambuliaji Emile Smith Rowe mwenye miaka 23, na kipa Aaron Ramsdale (25), kuondoka iwapo watapokea ofa kubwa. **(Mirror)**

**DRAGUSIN ATAJWA SPURS**

KLABU ya Tottenham Hotspur inatarajiwa kuongeza juhudi za kutaka kumnunua beki wa Genoa mwenye umri wa miaka 21, Radu Dragusin lakini watakabiliwa na ushindani kutoka kwa Roma. **(Telegraph)**

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI ULAYA




# RICE AKIRI ARSENAL KWA SASA IMEISHIWA NGUVU

●●● Inasikitisha sana, kushindwa mechi mbili za mwisho, ni ngumu kumeza...

**LONDON, England**

DECLAN Rice amekiri Arsenal hivi sasa imeishiwa nguvu baada ya kumaliza mwaka 2023 wakiwa na matokeo mabaya.

‚Washikabunduki‘ hao wa London Kaskazini, walipoteza kwa mabao 2-1 dhidi ya Fulham juzi Jumapili, huku wakitoka kufungwa 2-0 na West Ham, Alhamisi.

Rice mwenye umri wa miaka 24, aliwaonya wachezaji wenzake baada ya kuporomoka hadi nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi Kuu wakiwa wameongoza kipindi cha Krismasi.

Aliiambia Sky Sports: „Inasikitisha sana, ni ngumu sana kuipokea, ni wazi haitoshi kutoka kwetu.

„Matokeo mawili ya mwisho hayakuwa yale ambayo tumehitaji au tumekuwa tukiweka katika msimu huu.

„Tumekuwa tukifanya vema hadi mechi mbili zilizopita, hasa kutoka kwa sare ya Liverpool, tulihisi kama tunaweza kusonga mbele.

„Lakini baada ya kushindwa mechi mbili za mwisho, ni ngumu kumeza.“

Arsenal walitandikwa na klabu ya zamani ya Rice na juzi walishindwa tena kupata ushindi baada ya bao la mapema la Bukayo Saka.

Raul Jimenez alisawazisha baada ya kipindi ya mapumziko na Bobby Decordova-Reid akafunga bao la ushindi kipindi cha pili katika matokeo ambayo yalistahili kwa ‚Cottagers‘ hao.

Rice aliongeza: „Katika mchezo dhidi ya West Ham, tulipiga mashuti mengi, nafasi nyingi kwenye eneo la wapinzani na hatukuweza kufunga.

„Unapokuwa mbele kwa bao 1-0 unahitaji kudhibiti zaidi, kuwa na imani zaidi na nia.

„Mtazamo unahitaji kuwa bora, tunahitaji kudai zaidi kutoka kwa kila mmoja wetu kwa sasa.“

HABARI MICHEZO

# ALONSO KUFANYIWA UPASUAJI WA MGONGO




**BARCELONA, Hispania**

MLINZI wa Barcelona, Marcos Alonso, atafanyiwa upasuaji wa mgongo siku chache zijazo, klabu hiyo ilisema jana.

Klabu hiyo ya Katalunya ilisema upasuaji huo unalenga kutatua "matatizo katika eneo la kiuno" ambayo yamemweka nje Alonso mwenye umri wa miaka 33 katika wiki za hivi karibuni.

Barca walisema watatoa maelezo zaidi baada ya upasuaji huo kufanyika na hawakutoa ratiba ya kupona kwa Alonso.

Mchezaji huyo wa zamani wa Chelsea, amecheza mechi saba tu msimu huu, nne kama mchezaji wa kikosi cha kwanza.

Amecheza jumla ya mechi 44 akiwa na Barcelona, akifunga mabao matatu.

Barcelona ipo katika nafasi ya nne kwenye LaLiga - pointi saba nyuma ya viongozi Real Madrid na Girona baada ya mechi 18 -- na watacheza na Las Palmas siku ya Alhamisi.

# Ange akunwa Spurs kufunga mwaka 2023 kwa ushindi



**LONDON, England**

KOCHA Ange Postecoglou amefurahishwa na jinsi Tottenham Hotspur walivyokabiliana na matatizo msimu huu hasa kwenye suala la majeruhi na akaipongeza kwa ushindi wao wa mabao 3-1 wa juzi Jumapili.

Spurs ambao walikuwa na majeruhi wengi walimaliza mwaka 2023 kwa ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Bournemouth.

Kocha huyo aliwasifu nyota wake kwa morali yao huku vijana hao wa London Kaskazini wakisonga mbele na kupitwa pointi tatu na vinara wa Ligi Kuu England Liverpool, ambao wana mchezo mkononi.

Aliiambia Sky Sports: "Kila wiki ni vita na tulilazimika kupigana leo (juzi).

"Wakati huo huo, nilidhani tulicheza vitu vya heshima pia.

"Baada ya Brighton, nilisema wachezaji hawa wametoa kila kitu walichonacho na ni sifa kwao.

"Hatujaweza kuzunguka, lakini bado tunafanya maonesho na bidii.

"Tunajaribu kujenga kitu. Nina maumivu ya kuendelea kujirudia lakini tunajaribu kujenga timu ambayo inacheza tofauti kidogo na ina uimara fulani na unaweza kupata hiyo kupitia nyakati ngumu.

"Baadhi ya hayo ni kujitakia kwa kusimamishwa lakini tumekuwa na majeruhi wengi. Hatujataka kutoa visingizio na bado tuko ndani na kupigana.

"Tumepitwa pointi tatu na vinara waliopo kileleni, kwa hiyo ikiwa hiyo ndio tofauti kati ya kuwa na msimu mzuri na tulipo nitaichukua.

"Unapojaribu kujenga kitu bila shaka utakuja dhidi ya changamoto kadhaa.

"Naona maendeleo. Wakati mwingine hayaonekani na si soka au matokeo, wakati mwingine ni timu inayokua tu. Kulikuwa na ukuaji zaidi leo (juzi)."



# Carvalho mambo magumu, arejeshwa Liver

**LIVERPOOL, England**

FABIO Carvalho amerejea Liverpool baada ya muda wake wa mkopo katika Klabu ya RB Leipzig kukamilika mapema.

Winga huyo mwenye umri wa miaka 21, alijiunga na timu hiyo ya Ujerumani kwa mkopo wa msimu mmoja Juni, mwaka jana, lakini alianza mechi tatu pekee katika jumla ya mechi 15 kwenye mashindano yote ya timu hiyo kufikia msimu huu.

Mkurugenzi wa michezo wa Leipzig, Rouven Schroder alisema kwenye tovuti ya timu hiyo "pande zote mbili zilitarajia zaidi kutoka wakati wake hapa - hasa Fabio katika suala la muda wake wa kucheza."

"Kutokana na ubora na ushindani ndani ya kikosi chetu kwenye nafasi yake, hatuwezi kumhakikishia hili," alisema Schroder.

"Tulifanya majadiliano kadhaa katika siku za mwisho, tuliamua kumaliza mkopo wake mapema."

Carvalho, ambaye ameichezea Timu ya Taifa ya Ureno chini ya miaka 21, alihamia Liverpool kutoka Fulham msimu wa majira ya joto wa 2022 na amecheza mara 21 kwa 'Wekundu' hao akifunga mabao matatu.

HABARI MICHEZO

# OKRAH KUANZA YANGA NA WASUDAN MAPINDUZI LEO

Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR

BAADA ya kuichakaza 'mkono' mabao 5-0 timu ya Jamhuri ya Zanzibar, miamba ya soka Tanzania Bara, Yanga itashuka tena dimbani leo kwenye mechi yao ya pili ya Kombe la Mapinduzi dhidi ya Jamus FC ya Sudan Kusini huku kila moja ikipania ushindi ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kuunyemelea ubingwa huo.

Wakizungumza katika mkutano waandishi wa habari jana baada ya kumaliza kikao cha maandalizi wa mchezo wao huo, makocha wa timu hizo walisema wanahitaji kushinda ili kujiweka katika mazingira mazuri ya kusonga mbele kwenye mashindano hayo.

Kocha Msaidizi wa Yanga, Msenegal Moussa N'Daw, amesema pamoja na kuwa jana walipata matokeo ya mabao 5-0 dhidi ya Jamhuri, lakini leo wanahitaji ushindi pia ili kujiweka katika mazingira mazuri ya kuendelea katika hatua inayofuata ya michuano hiyo.

Alisema katika mchezo huo wa leo mashabiki wa Yanga wawe na matarajio ya kumuona uwanjani mshambuliaji mpya alietambulishwa juzi usiku, Augustine Okrah, kwa kuwa atakuwamo katika orodha ya kikosi kitakachocheza.

"Okrah juzi tu alitambulishwa na ni matumaini yangu kwamba kesho (leo), atakuwamo katika orodha ya wachezaji watakaocheza," alisema.

Sambamba na hayo alisema kuwa baada ya mchezo wao wa awali dhidi ya Jamhuri, kuna makosa ambayo wameyaona na tayari wameyafanyia kazi.

Naye mwakilishi wa wachezaji, Zawadi Mauya, alisema kwa kiasi kikubwa matayarisho kuelekea mchezo huo yamekuwa mazuri baada ya juzi kumaliza mechi kwa ushindi mkubwa.

Alisema anamini kila mchezaji wa timu yao yupo vizuri kwa ajili ya mechi ya leo licha ya kwamba hawajawahi kukutana na timu hiyo kutoka Sudan Kusini.

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa Jamus FC, John Alier, alisema Yanga ni timu kubwa na ni maarufu katika soka la Afrika, lakini wamejiandaa kuhakikisha wanashinda mchezo huo.

"Tunajua kwamba tunacheza na timu kubwa, lakini hakuna mwalimu ambae anaikatia tamaa timu yake, tumejipanga kwa mchezo huu, ili tushinde hasa baada ya mechi zetu mbili kutopata matokeo mazuri,"alisema.



Kiungo wa Yanga, Jonas Mkude (kushoto), akimpongeza mshambuliaji wa timu hiyo, Clement Mzize, baada ya kuifungia timu yake bao la tano wakati wakishinda 5-0 dhidi ya Jamguri FC, kwenye mechi ya Kombe la Mapinduzi iliyopigwa Uwanja Amaan Sports Complex juzi. Pembeni ni Chrispin Ngushi. **MPIGAPICHA WETU**

## Simba, Yanga sasa ni shusha ni shushe

INATOKA UK. 24

mchezaji huyo ambaye anacheza nafasi ya ushambuliaji na wakati mwingine kama winga wa kushoto, ni mmoja wa wachezaji ambao wamepitishwa kusajiliwa na kocha Abdelhak Benchikha, akiwapiga chini Victorien Adebayor na Cesar Manzoki ambao tayari walikuwa na mazungumzo ya awali na klabu tangu huko nyuma kusajiliwa kupidi hiki cha dirisha dogo.

"Kibao kimegeuka, Benchika amewakataa kwa madai kuwa hawajacheza kwa muda mrefu kwa hiyo hawatakuwa na msaada kwa timu kwa sababu itabidi wapate muda mrefu wa kuwa fiti, badala yake anataka wachezaji ambao kwa sasa wanacheza ili wakija waendelee na moto ule ule kwani hana muda wa kupoteza, kuna Ligi Kuu na Ligi ya Mabingwa," kilieleza chanzo chetu ndani ya klabu hiyo.

Imedaiwa kuwa Benchika pia ndiye aliyewakata Aubrey Modiba wa Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini kutokana na usajili wake kuwa mgumu na unaweza kuchukua muda mrefu, pamoja na Ibrahim Imoro aliyemaliza mkataba wa Al Hilal ya Sudan kuwa hayupo fito kwa kutocheza kwa muda mrefu, badala yake akamtaka Hernest Briyock Malonga anayeichezea Klabu ya CSMD Diables Noirs ya Congo Brazaville kwa sababu ya umri mdogo wa miaka 21, lakini pia akicheza kila wiki na timu yake.

Kwa upande wa Yanga baada ya juzi kutabulisha usajili wao mpya, kiungo mshambuliaji Augustine Okrah, uongozi wa Yanga umesema hawajafunga usajili, badala yake wanatarajia kumtangaza mchezaji mwingine anayecheza nafasi ya ushambuliaji.

Ingawa haukutaja jina la mshambuliaji huyo, lakini habari kutoka chanzo chetu ndani ya klabu hiyo, zimeeleza kuwa ni Leonel Ateba kutoka Klabu ya Dynamo FC de Douala ya Cameroon, na amekubali kusaini mkataba wa miaka miwili huku kwa sasa akiwa katika majukumu ya timu yake ya taifa kujianda na fainali za AFCON, mwaka huu nchini Ivory Coast.

Yanga ipo sokoni kusaka mshambuliaji asilia, kutokana kukosa mabao katika idara hiyo na imekuwa ikiwategemea zaidi viungo Stephane Aziz Ki, ambaye anaongoza kwa mabao ndani ya Ligi Kuu Bara akifunga 10, Maxi Nzengeli (mabao 7), kisha Pacome Zouzoua (mabao 4). Kwa upande wa washambuliaji, Kennedy Musonda amefunga matatu, Hafiz Konkoni na Clement Mzize wakicheka na yavu mara moja tu.

Usajili wa Ateba ni kwa ajili ya kuongeza nguvu kwenye safu hiyo na anakuja kuchukuwa nafasi ya Hafiz Konkoni ambaye ameshindwa kukata kiu ya Wanajagwani hao ambao waliamini anakuja kuvaa vema viatu vya Fiston Mayele.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema baada ya kufanikiwa kumtambulisha Okrah, kazi bado inaendelea na wanaleta mtu hatari eneo la ushambuliaji ambaye anakuja kuimarisha safu hiyo.

Alisema miaka yote wanafanya usajili, lakini msimu huu wanafanya usajili bora kwa sababu wanakuja wachezaji hatari hasa kwenye safu ya ushambuliaji.

"Tumemtambulisha Okrah ambaye hatutaki kumpa presha tunaacha miguu yake iongee, lakini hatutaishia kwa huyo rais wa Yanga, Hersi Said ameniambia kuna kifaa kingine kinatua nchini," alisema.

## Kocha Stars atema cheche, akianika majembe ya Afcon

INATOKA UK. 24

Salum, Mudathir Yahya, Morice Abraham, Himid Mao, Tarryn Allarakhia na Twariq Ahmed.

Kwa upande wa washambuliaji ni Mbwana Samatta, Simon Msuva, Kibu Denis, Abdul Suleiman, Ben Starkie, Charles Mmombwa, Khlefin Hamdoun na Cyprian Kachwele.

Kikiwa nchini Misri, Kocha Amrouche atakiongoza kucheza mechi tatu za kirafiki na kisha atafanya mchujo kupata wachezaji 27 ambao wataenda Ivory Coast tayari kwa michuano ya AFCON ambapo kitatupa karata yake ya kwanza Januari 17 dhidi ya Morocco. Stars ipo Kundi E pamoja na Morocco, DR Congo na Zambia.

Akizungumza na Nipashe jana, Amrouche alisema anaimani na wachezaji aliowaita na anatambua Tanzania kuna vipaji na nyota wazuri, lakini amekuwa na chaguo lake kulingana na michezo iliyopo mbele yao.

Alisema Kelvin ni mchezaji mzuri na amekuwa akipata nafasi ya kucheza KRC Genk, lakini hakumuita kwa sababu hayuko kwenye mipango yake na aliwahi kumuita Bacca ambaye hakuwa akipata nafasi katika klabu yake ya Yanga, ila alimwamini na kuonesha maajabu.

"Ninaimani na wachezaji wangu, tunaemda kupambana kutafuta matokeo mazuri katika michuano ya AFCON, tunaenda Misri kuweka kambi pamoja na kucheza mechi tatu za kirafiki, moja dhidi ya Timu ya Taifa ya Misri.

"Baada ya mechi hiyo tutacheza mechi mbili zingine, baadaye tunaenda Ivory Coast na tayari kwa michezo yetu. Ninawaheshimu wapinzani wetu, ila tunaenda kwa ajili ya kushinda," alisema Amrouche

Aliongeza kuwa falsafa yake ni ushindi na hata wachezaji wanatambua kuwa hapendi kupoteza kwa sababu akifungwa anaugua, hivyo matarajio yake ni kuhakikisha wachezaji wanapambana kupata matokeo mazuri.



Amrouche

Michezo
Jumanne Januari 2, 2024
Nipashe

Rice akiri Arsenal sasa imeishiwa nguvu UKURASA 21



# SIMBA SC, YANGA SASA NI SHUSHA NI SHUSHE

## Zatingisha anga la usajili, ndege zapishana kushusha majembe, huku...

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

ACHANA na ilichofanya Klabu ya Simba ambacho watani wao wa jadi, Yanga walikifanya, kwa kusajili mchezaji kutoka JKU ya Zanzibar, baada ya Wekundu wa Msimbazi hao jana nao kumtambulisha kiungo mshambuliaji Saleh Karabaka kutoka klabu hiyo, ikisema atakuwapo Msimbazi kwa misimu mitatu.

Mchezaji huyo ametambulishwa rasmi jana na kuwa mchezaji wa kwanza kusajiliwa kwenye kipindi cha dirisha dogo msimu huu ndani ya klabu hiyo.

Hiyo ikiwa ni baada ya katikati ya mwezi Desemba mwaka jana, Klabu ya Yanga kumsajili mchezaji mwingine wa JKU ambaye naye pia anacheza nafasi ya kiungo mshambuliaji, Shekhan Ibrahim Hamisi, ambaye naye aliingia kwenye rekodi ya kuwa wa kwanza kusajiliwa na klabu hiyo baada ya kipindi cha dirisha dogo la usajili kufunguliwa Desemba 16, mwaka jana na likitarajiwa kufungwa Januari 15, mwaka huu.

Simba ikizungumzia usajili huo ilisema: "Usajili wa Karabaka mwenye umri wa miaka 23, unakuwa wa kwanza katika dirisha hili dogo.

"Karabaka tayari amejiunga na timu Visiwani Zanzibar na ataanza kuonekana akiwa na jezi ya Mnyama katika michuano ya Mapinduzi inayoendelea. Pamoja na uwezo alionao Karabaka jambo jingine lililotuvutia ni umri wake mdogo ambao tunaamini atakuwa msaada mkubwa kwa timu."

Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu hiyo, Ahmed Ali alisema wachezaji wote ambao watawasajili ni ushauri wa benchi la ufundi na si vinginevyo.

"Tukimsajili mchezaji kutoka sehemu yoyote tutakwambia huyu tumeshauriwa na nani, na pia benchi la ufundi ni lazima lihusike," alisema Ahmed ambaye ameweka wazi kuwa usajili utaendelea.

Wakati hayo yakiendelea, klabu hiyo leo inatarajiwa kumpokea Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere, mchezaji wake mpya Mauricio Cortes Nunez mwenye umri wa miaka 26 raia wa Colombia kwa ajili ya kukamilisha taratibu za mwisho za usajili.

Habari kutoka ndani ya klabu hiyo zimeeleza kuwa

INAENDELEA UK. 23



Mauricio Cortes

# Kocha Stars atema cheche, akianika majembe ya Afcon

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Taifa Stars, Adel Amrouche, amefunguka juu ya kuwaita wachezaji ambao hawapati nafasi katika timu zao akiamini wanauwezo wa kuonyesha maajabu kama ilivyokuwa kwa beki wa Yanga, Ibrahim Abdulla 'Bacca', alipomuita kwa mara ya kwanza.

Kauli hiyo aliitoa jana wakati akitangaza kikosi cha wachezaji 31 huku Kelvin John anayeichezea KRC Genk ya Ubelgiji na Clement Mzize wa Yanga, akiwaacha katika kikosi chake kitakachokwenda kupeperusha bendera ya Tanzania kwenye Fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) 2023, zitakazofanyika nchini Ivory Coast kuanzia Januari 13, mwaka huu.

Kikosi hicho cha wachezaji 31 kilichoondoka jana mchana kuelekea nchini Misri kwa kambi ya wiki moja kabla ya kuunganisha kwenda Ivory Coast tayari kwa fainali hizo, kinaundwa na makipa; Aishi Manula, Beno Kakolanya, Metacha Mnata na Kwesi Kawawa.

Mabeki ni Dickson Job, Ibrahim Abdulla 'Bacca', Bakari Mwamnyeto, Lusajo Mwaikenda, Haji Mnoga, Abdi Banda, AbdulMalik Zakaria, Mohamed Hussein 'Tshabalala', Miano Danilo na Novatus Dismas.

Viungo ni Mzamiru Yassin, Moe Sagat, Sospeter Bajana, Feisal

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >